# Nipashe

Alhamisi Novemba 5, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580390

The Guardian digital

nipasheTZ

0745 700710





UKURASA 11

**MWINYI** azibana Bandari na TRA kuhusu utendaji



UKURASA 3

**KASI** ya umeya, wenyekiti wa halmashauri yapamba moto

UKURASA 4

# Wakuu 20 mashuhuda Magufuli akila kiapo

Wamo marais watatu, mabalozi, maandalizi yakamilika, TB Joshua ndani ...

*Endelea Uk. 2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua maandalizi ya Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana, utakaotumika kumwapisha Rais Dk. John Magufuli leo. Wengine ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, IGP Simon Sirro na Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Diwani Athuman. **PICHA: OWM**

# Trump atishia kupinga matokeo urais kortini

UKURASA 2

## Ndugai, Tulia wapata wapinzani

UKURASA 3


SALAMU ZA PONGEZI



Gazeti Nipashe linampongeza Rais Dkt John Magufuli na Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha Miaka 5. 2020 - 2025

Kwa salamu za pongezi
Wasiliana nasi kwa Simu: 0686 101335
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



SALAMU ZA PONGEZI



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati), akizungumza na Viongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na Viongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar katika ukumbi wa Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Wakuu 20 mashuhuda Magufuli akila kiapo

## ■TB Joshua naye apeleka upako Dodoma

**Na Waandishi Wetu, DODOMA**

VIONGOZI wakuu wa nchi 20 leo wanatarajiwa kuhudhuria sherehe za kuapishwa Rais Mteule wa Tanzania, Dk. John Magufuli, wakiwamo marais kutoka nchi za Uganda, Zimbambwe na Visiwa vya Comoro.

Tukio hilo la kihistoria ambalo ni mara ya kwanza kufanyika mkoani Dodoma tangu nchi ipate uhuru, pia litashuhudiwa na mabalozi wa nchi 83.

Pia, wanatarajiwa kuwapo viongozi wenye hadhi ya juu barani Afrika akiwamo Rais mstaafu wa Nigeria, Olusegun Obasanjo na mhubiri maarufu duniani, TB Joshua wa Nigeria.

Akizungumza jana na waandishi wa habari katika Uwanja wa Jamhuri ambao ndiyo sherehe hizo zitafanyika, Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, aliwataja marais watakaokuwapo kuwa ni Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, Rais wa Visiwa vya Comoro, Azali Assoumani na Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa.

Aliwataja viongozi wengine wakuu wa nchi hizo 20 kuwa ni pamoja na mawaziri wakuu, makamu wa rais wa nchi mbalimbali za Afrika, Waziri wa Mambo ya Nje wa Qatar ambaye atamwakilisha Mfalme wa nchi hiyo na mawaziri ambao watawakilisha nchi zao.

"Hawa ni wageni wa hadhi ya juu wa serikali na tunaendelea kupokea uthibitisho, lakini nchi mbalimbali duniani zitawakilishwa na mabalozi wao waliopo nchini.

"Hadi leo (jana) mchana, mabalozi 83 wamethibitisha na tumealika viongozi wengine wa ndani ya nchi; mawaziri, manaibu waziri wanaomaliza muda wao," alisema.

**UKOMO BARAZA LA MAWAZIRI**

Alifafanua kuwa kwa mujibu wa Katiba, leo Rais atakapokula kiapo, mawaziri wote baada ya kiapo hicho utendaji wao utakuwa umekoma.

Pia, alisema watakuwapo makatibu wakuu, watendaji mbalimbali wa taasisi na wadau wengine wa serikali.

Alisema viongozi waalikwa wakiwamo mawaziri, manaibu waziri, makatibu wakuu, manaibu makatibu wakuu, wakurugenzi wa sekta binafsi, taasisi za umma, viongozi wa dini, majaji na viongozi wa vyama vya siasa wataingia kwa mabasi maalum uwanjani na magari yao watatakiwa kuegeshwa kwenye Bustani ya Chinangali iliyoko jirani na Uwanja wa Ndege wa Dodoma na kupanda mabasi hayo.

"Basi la kwanza litaondoka saa 12:30 asubuhi na viongozi hawa wanatakiwa kuzingatia, watakaoruhusiwa magari yao kuingia uwanjani viongozi ambao wapo kiitifaki na viongozi waliokuja kuwakilisha nchi zao," alisema.

Alisema shughuli hiyo pia itakuwa na gwaride la kiapo ambalo litaongozwa na vikosi vya Jeshi na Ulinzi.

**WASANII KUPAMBA**

Dk. Abbas alisema sherehe hiyo itapambwa na burudani kuanzia asubuhi wakiwamo wasanii wa muziki wa kizazi kipya ambao wameandaa wimbo maalum wa mitano tena.

Aliwataja wasanii wao kuwa ni pamoja na Nasib Abdul, maarufu Diamond Platnumz, Rajab 'Hamonies', Ali Kiba, Faustina Mfinanga 'Nandy', Zuhura Kopa 'Zuchu', Dula Makabila, Sholo Mwamba, Mrisho Mpoto, Kala Jeremiah pamoja na wasanii wa ngoma za asili za Tanzania Bara na Zanzibar.

"Wananchi wawahi asubuhi kwenye mageti watakayoelekezwa na kukaa kwenye maeneo yanayowahusu na mageti yatakuwa wazi kuanzia saa 12 asubuhi na kutokana na uwanja ulivyo, wananchi wengine watakaa maeneo ya nje yameandalia na kuangalia kupitia 'screen' (kiambaza)," alisema.

Msemaji huyo alisema pia kuna maeneo yameandaliwa kwa ajili ya wananchi watakaokosa kuingia uwanja wa Jamhuri ambapo watawekewa kiambaza kwa ajili ya kuona kinachoendelea ndani.

Maeneo hayo ni pamoja na Uwanja wa Barafu na Uwanja wa Shule ya Sekondari Central.

Vilevile, alisema viongozi wa kitaifa wataanza kuingia uwanjani kuanzia saa mbili hadi saa tatu asubuhi na baadaye ratiba zingine zitaendelea.

**BARABARA KUFUNGWA**

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema kutokana na uwapo wa tukio hilo baadhi ya barabara zitafungwa kwa muda na kuwaomba wananchi kuvumilia hali hiyo.

Alisema kutokana na tukio hilo kufanyika Dodoma kwa mara ya kwanza, ni vyema wananchi wakajitokeza kwa wingi kushuhudia sherehe hizo za kihistoria.

**ULINZI KUIMARISHWA**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema ulinzi na usalama umeimarishwa kwa wananchi na viongozi wote watakaohudhuria sherehe hizo.

"Waje Dodoma ni salama, tumejipanga kuhakikisha wote wanahudumiwa kiusalama na hakuna atakayechukuliwa hata pochi, jana(juzi) tulikagua nyumba za kulala wageni ili kuhakikisha wanaoingia na kutoka ni wageni salama,"alisema.

Oktoba 28, mwaka huu, ulifanyika uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani ambapo Rais Magufuli aliomba ridhaa ya kuongoza tena kwa miaka mitano mingine na kutangazwa mshindi kwa kupata asilimia 84.4 ya kura zilizopigwa.

Chama chake, Chama Cha Mapinduzi (CCM) pia kiliibuka na ushindi mkubwa kikishinda kwa zaidi ya asilimia 90 ya majimbo na kata zote nchini.

Kilichokuwa chama kikuu cha upinzani katika Bunge lililopita, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimeambulia jimbo moja tu kati ya majimbo yote 264.

Vyama vingine vilivyochomoza katika kuchukua majimbo hayo mbali na CCM na CHADEMA, ni ACT-Wazalendo kilichopata majimbo manne (yote Zanzibar) na Chama cha Wananchi (CUF) kilichoambulia jimbo moja Tanzania Bara na mawili visiwani Zanzibar.

***Imeandikwa na Agusta Njoji na Gwamaka Alipipi.***

# Trump atishia kupinga matokeo mahakamani

**WASHINGTON, Marekani**

DONALD Trump amepanga kwenda mahakama ya juu zaidi kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu wa Marekani uliofanyika juzi.

Kukiwa bado kura nyingi hazijahesabiwa, Trump, alidai kuwa ameshinda. Hadi jana mchana, majimbo 40 kati ya 50 yaliyohesabiwa kura zake, Biden alikuwa akiongoza kwa kura 220 huku Trump akiwa na kura 213.

"Ukweli ni kwamba tumeshinda," Trump alidai hivyo bila ya kuwa na ushahidi wowote.

Trump ambaye anatetea nafasi yake ya Rais nchini humo, alidai kuwa uchaguzi umekumbwa na udanganyifu.

"Hii ni aibu kwa nchi yetu," alisema Trump na kuongeza kwamba anapanga kwenda mahakama ya juu zaidi kupinga matokeo ya uchaguzi.

Mamilioni ya kura katika uchaguzi huo zilikuwa bado hazijahesabiwa, hivyo Rais hana haki yoyote ya kujitangaza mshindi.

Kuwa Rais wa Marekani huna haja ya kushinda kwa kura nyingi, badala yake mgombea anahitajika kushinda kura ya wajumbe ambapo kila jimbo lina kura au wajumbe kulingana na idadi ya watu.

Kwa ujumla kuna kura 538 za majimbo na yule atakayepata angalau 270 ndio anakuwa Rais.

Wachambuzi wa Republicans na wenye msimamo mkali hata hivyo wameonyesha wasiwasi wao kuhusiana na matamshi ya Trump.

Akizungumza na Shirika la Habari la ABC News, aliyekuwa Gavana wa New Jersey na mshauri wa Trump, Chris Christie ameitaja hatua ya kiongozi huyo anayetetea nafasi yake ya urais kama isiyofaa hata kimkakati kwake kama Rais.

"Ni uamuzi mbaya. Ni uamuzi mbaya wa kisiasa." Rick Santorum, aliyekuwa Seneta wa Republican kutoka Pennsylvania, alisema kwamba matamshi ya Trump yamemsababishia msongo wa mawazo.

"Kwa kutumia neno udanganyifu... kwangu naona ni makosa," alisema hivyo akizungumza na CNN.

Kura majimboni zilionyesha katika Jimbo la Florida, lilinyakuliwa na Trump, ambako wengi ni raia wa Marekani wenye asili ya Cuba katika kaunti ya Miami-Dade wanaomuunga mkono.

Jimbo la Arizona limekuwa likipigia kura Chama cha Republican tangu mwaka 1996, lakini inaonekana kwamba huenda likachukuliwa na Biden.

Kwa upande wa majimbo ya Wisconsin na Pennsylvania, yalikuwa bado hayajaanza kuhesabu kura zilizopigwa kwa njia ya posta, shughuli ambayo huenda ikachukua siku kadhaa.

***BBC***



## HABARI KITAIFA

# 10 wajitokeza kuchuana na Ndugai, Dk. Tulia

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WANACHAMA 10 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamejitosa kuomba kuteuliwa na chama hicho kuwania uspika na unaibu spika wa Bunge la Tanzania, huku mmoja akijitoa dakika za mwisho.

Waliojitosa ni Spika wa Bunge la 11 Job Ndugai na Naibu Spika Dk. Tulia Ackson ambao wanatetea nafasi zao.

Wengine ni David Meshack, ambaye alikuwa mtiania ubunge jimbo la Kibamba, mkoani Dar es Salaam ambaye alishika nafasi ya 36 katika kura za maoni ndani ya chama; Stamina Mdolo na Barua Mwakilanga ambaye ni mwanasheria mbobezi.

Hata hivyo, waliochukua fomu Ofisi ndogo ya CCM Dar es Salaam majina yao hayajapatikana huku aliyechukuliwa Ofisi ya Zanzibar Abdallah Mwinyi akijitoa kuwania uspika.

Akizungumza jana na waandishi wa habari baada ya kuchukua fomu, Meshack alisema nia yake ni kupata fursa ya kuwatumikia wabunge pamoja na Watanzania.

"Siyo kama na mpinga Spika Ndugai kuchukua nafasi hii hapana, lengo langu ni kuwatumikia Watanzania kama nilishindwa kwenye kura ya maoni... hii pia ni nafasi yangu ya kutaka kutimiza kile nichotaka kuwafanyia Watanzania,"alisema Meshack.

Alisema kama atapata fursa ya kuchaguliwa kuwa Spika, atahakikisha bunge hilo linakuwa la viwango ambalo litaendeshwa kwa kuzingatia kanuni.

Akizungumza baada ya kuhitimisha utoaji fomu, Katibu Msaidizi Mkuu, wa Organizesheni CCM Taifa, Solomon Itunda, alisema mpaka jana mchana jumla ya wanachama waliochukua fomu walikuwa 10.

Hata hivyo, alisema kuwa wanachama wengine ambao yeye hana majina yao wamechukua fomu ofisi ndogo ya CCM, Dar es salaam.

Juzi, Katibu Mkuu wa CCM, Dk.Bashiru Ali, alisema kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM kitaketi kesho kwa ajili ya kupitisha jina la Spika na Naibu Spika.

# Dk. Mwinyi azibana Bandari na TRA

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ameutaka uongozi wa bandari na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhakikisha kazi za kulitumia ghala jipya la mizigo lililoko Saateni zinaanza mara moja ili kupunguza mrundikano wa makontena katika Bandari ya Malindi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Saateni, Zanzibar baada ya kutembelea ghala jipya la mizigo lililojengwa na kampuni ya serikali na kuagiza kutumika haraka ghala hilo na kwamba hatua hiyo itapunguza mlundikano wa makontena katika bandari ya Malindi.

Pia alikemea akikemea tabia ya kufanya kazi kwa mazoea kutokana na kampuni hiyo ya ujenzi kuchukua muda mrefu wa ukamilishaji wa ghala hilo.

Rais Mwinyi alisikitishwa na hali hiyo ya kuchelewa kukamilika kwa ghala hilo hasa ikizingatiwa kwamba wajenzi ni kampuni ya serikali ambayo watendaji wake wakuu ni askari wa Idara Maalum za SMZ.

Alisema utendaji kazi kwa mazoea ndio uliosababisha kulundikana kwa makontena katika bandari ya Malindi na kueleza kuwa fedha za serikali zimepotea kutokana na ufanisi wa bandari kutoridhisha.

Kutokana na hali hiyo, aliutaka uongozi wa Mamlaka ya Bandari kutoa kazi kwa muda maalum na fedha maalum, kutokufanya hivyo kunasababisha uvunjifu wa utaratibu wa serikali kuilipa kampuni fedha zote na matokeo yake kukaa miezi mitatu kwa kujenga waya wa umeme wa usalama uliozunguka kuta za ghala hilo.

Alisema jambo hilo halivumiliki na meli katika Bandari ya Zanzibar haziji na zinazokuja zinakawia kushusha mizigo hatua ambayo inatokana na uzembe na hatimaye kusababisha upotezaji wa mapato.

Pia alisisitiza kuanza kazi mara moja ya kuweka mizigo katika ghala hilo huku akishanganzwa na maelezo ya Msimamizi wa Ujenzi huo, Hassan Sarboko kutoka Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kumaliza ujenzi huo miezi mitatu iliyopita bila ya kukabidhi kwa wahusika.

Naibu Kamishna wa TRA Zanzibar, Mcha Hassan Mcha, na Kaimu Mkurugenzi Ufundi wa Shirika la Bandari Zanzibar, Salum Udi, waliahidi kuanza kazi kesho ya kuweka mizigo katika ghala hilo baada ya kuhakikishiwa na msimamizi wa ujenzi kwamba ghala limekamilika.

Awali, Dk. Mwinyi alikutana na uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji , Wizara ya Fedha na Shirika la Bandari pamoja na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi huko Ikulu Jijini Zanzibar.

Mkutano huo ulifanyika kujadili hatua mbalimbali zitakazoleta jibu la kuwapo ufanisi katika Shirika la Bandari ya Zanzibar ambao umeelezwa kuwa umezorota.

Kukutana na viongozi hao kunatokana na ziara yake aliyoifanya juzi katika Bandari ya Malindi na baada ya kuelezwa hali ya utendaji, aliagiza kukutana na uongozi huo.

Alisema kutokana na bandari ya Zanzibar kuwa kitovu cha biashara, ni lazima kufanyike utaratibu wa kuondosha changamoto hizo kwa haraka.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII

SALAMU ZA PONGEZI





Kamati ya Taifa YA Uongozi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF, inakupongeza Mhe. **Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufuatia ushindi mkubwa ulioupata katika uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 . TASAF inaahidi kuunga mkono dhamira yako ya kuboresha maisha ya wananchi kupitia utekelezaji wa Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya TASAF.

*Pamoja Tuondoe Umaskini*

Mkurugenzi Mtendaji
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF**
Barabara ya Jakaya Mrisho Kikwete,S.L.P 2719, Dodoma, TANZANIA,
Simu:**+255 26 2963866**, Nukushi:+255 26 2963871,
Barua pepe: **info@tasaf.go.tz**, Tovuti: **www.tasaf.go.tz**

215975901

# Kinyang'anyiro umeya, uenyekiti wapamba moto

**Na Waandishi Wetu**

MADIWANI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wameendelea kupigana vikumbo katika mbio za kuwania umeya na uenyekiti katika halmashauri kadhaa nchini.

Mbio za madiwani wa chama hicho zinatokana na kuibuka na ushindi mkubwa wa urais, ubunge na urais katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu na kuvifanya vyama vya upinzani kukosa sifa ya kuwania kutokana na kutokuwa na madiwani wachache sana.

**BUKOBA**

Watiania 20 wa nafasi ya umeya, uenyekiti, naibu meya na makamu mwenyekiti wamejitokeza kuchukua fomu kwenye ofisi za CCM katika Halmashauri ya Manispaa Bukoba na Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera. Wagombea hao ni madiwani wa waliochaguliwa Oktoba 28, mwaka huu. Katika kata za Halmashauri ya Bukoba kuna kata 29, kati ya hizo 26 zilikwenda CCM) na tatu upinzani.

Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba ina kata 14, ambapo kata 13 zinashikiliwa na CCM, moja upinzani.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Bukoba, Katibu wa CCM Bukoba Mjini, Flata Katumwa, alisema waliochukua fomu ya umeya ni sita na watano nafasi ya naibu meya.

Katibu wa CCM Halmashauri ya Wilaya Bukoba, Paul Mwita, alisema wagombea tisa nafasi ya uenyekiti, huku watano wakijitokeza nafasi ya makamu mwenyeviti.

**KIBAHA MJINI**

Katika Halmashauri ya Kibaha Mjini mkoani Pwani, madiwani wamechangamkia nafasi ya uenyekiti, Katibu wa CCM Kibaha Mjini, Hafidu Luambano, aliwataja waliochukua fomu za kuwania nafasi ya mwenyekiti ni saba, huku ya makamu wakijitokeza wawili.

Luambano aliwataja waliojitokeza kwa uenyekiti ni Focus Bundala, Musa Ndomba, Karim Mtambo, Judith Mluge, Raymond Chokala, Mwinami Simbawani na Leonard Mlowe, anayetetea nafasi yake.

Katika nafasi ya makamu mwenyekiti waliochukua fomu ni Selina Wilson na Judith Mluge.

Chama tawala kimeongeza muda kwa watia nia kuchukua fomu hizo hadi leo.

***Imeandikwa na Restuta Damian, Bukoba na Julieth Mkireri, Kibaha***



Mwonekano wa stendi mpya ya mabasi ya mikoani inayoendelea kujengwa katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waliodaiwa kuchochea kushambulia askari wanyamapori waachiwa huru

**Na Asraji Mvungi, MWANGA**

WATENDAJI wa vijiji katika Kata ya Kwakoa, Mwanga mkoani Kilimanjaro waliokuwa wamekamatwa kwa tuhuma za kuchochea wananchi kuwashambulia askari wa wanyamapori wameachiwa huru.

Watendaji hao, Abdalah Hasani wa Kijiji cha Kwakoa, Hashim Waziri wa Kijiji cha Ngulu na Salehe Juma wa Kitongoji cha Mkongea, walikamatwa baada ya kutokea mauaji ya Mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Kwangu.

Mwalimu huyo aliuawa na tembo baada ya wananchi kuwazuia askari wa Kikosi cha Kupambana na Ujangili (KDU) Kanda ya Kaskazini kuchukua mwili wa ndugu yao wakishinikiza tembo waliofanya mauaji nao wauawe.

Hata hivyo, baadaye viongozi hao wakishirikiana na wadau mbalimbali, waliwatuliza wananchi hao na taratibu za kuchukua mwili huo zikafanyika.

Akizungumzia tukio hilo, mmoja wa viongozi wa KDU Kanda ya Kaskazini, Goodluck Nnko, amewataka wananchi kutoa ushirikiano katika kukabiliana na makundi ya tembo yaliyovamia maeneo hayo, kazi inayofanywa na watendaji wa idara za wanyamapori badala ya kupambana nao.

Akizungumza na Nipashe juu ya hatua iliyofikiwa ya kuwadhibiti wanyama hao, Nnko amesema pamoja na idadi kubwa ya wananchi kuendelea kutoa ushirikiano, baadhi yao wamekuwa wakiwashutumu askari kwa mambo yaliyoko nje ya uwezo wao na pia kinyume cha sheria jambo linalodhoofisha jitihada zao.

"Bado tunaendelea na kazi ya kukabiliana na wanyama hawa na tunaamini tutafanikiwa. Lakini wako baadhi ya wananchi ambao wanataka kutumia njia za mkato na wengine wanafikia hatua ya kutaka kuwashambulia askari badala ya kuwapa ushirikiano," alisema Nnko.

Hata hivyo alisema wanaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kufuata sheria wakati wa kukabiliana na tembo na wengi wanaelewa na wasioelewa wameanza kuchukuliwa hatua.

"Juzi yalipotokea mauaji ilibidi baadhi ya viongozi wa vijiji wakamatwe baada ya kubainika kuwachochea wananchi kushambulia magari na askari wetu waliokuwa wanataka kuchukua mwili wa marehemu suala ambalo ni kinyume cha sheria. Lakini nashukuru kuwa wamekiri makosa na wameachiwa, lakini kiukweli walichofanya si sawa," alisema.

Kuhusu tuhuma hizo, Diwani wa Kwakoa, Kiende Mvungi, alisema kimsingi wananchi wote wako tayari kutoa ushirikiano wa kuwadhibiti wanyama hao na tofauti zilizokuwa zimetokea zilichangiwa na taharuki iliyokuwa imetawala katika eneo hilo na kwamba kwa sasa hali ni shwari na kazi ya kuwakabili tembo inaendelea.

"Tumeshakaa kwenye vikao na tumeshayamaliza na tunaendelea kuunganisha nguvu kati ya wananchi na watendaji wa wanyamapori kuhakikisha tunawadhibiti tembo hawa," alisema.

Hadi sasa licha ya kwamba hali ya usalama katika maeneo hayo ni shwari makundi ya tembo yameendelea kuonekana mitaani nyakati za jioni, usiku na alfajiri.

# Neema kujengwa kiwanda korosho

**Na Edina Elex, SINGIDA**

KAMPUNI ya Ward Holdings International (WHI) ya Marekani, imetangaza kuanza kujenga kiwanda kikubwa cha kubangua korosho Manyoni mkoani Singida jambo litakalosaidia kukuza uchumi kwa wakulima wa zao hilo mkoani hapa.

Rais wa WHI Kanda ya Africa, Godfrey Simbeye, alisema hayo jana baada ya kutembelea shamba la Masigati, wilayani Manyoni lenye ukubwa wa ekari 22,000 ambalo linajumuisha zaidi ya wakulima 700.

Simbeye alisema kiwanda hicho kitakachojengwa wilayani humo, kitakuwa cha mfano hapa nchini.

"Kampuni hii iko tofauti na kampuni zingine kwasababu ikiuza korosho nje ya nchi, lile gawio la faida linarudi kwa mkulima na litamneemesha mkulima wa Singida," alisema Simbeye.

Baada ya Wilaya ya Manyoni kuanza uzalishaji wa korosho, tayari wawekezaji wanne wameonyesha nia ya kujenga viwanda ikiwamo WHI amabayo inataka kujenga kiwanda kikubwa ambayo italiongezea thamani kwa ajili ya soko la Ulaya.

Mkurugezi Mtendaji wa Halmashauri ya Manyoni, Charles Fussi, ameonyesha kufurahishwa na uanzishwaji wa kiwanda hicho kwa kuwa kitawasaidia wakulima wa zao hilo kupata soko la uhakika .

Alisema kampuni hiyo tofauti na kampuni zingine zilizowahi kufika wilayani humo kwa ajili ya kuwekeza kwa kuwa haina masharti magumu ya kumbana mkulima.

"Kampuni ya WHI nimeona iko 'serious' (makini) katika kufanya kazi na sisi hususani katika zao la korosho. Ninaona wakulima watakavyokuwa mabilionea," alisema Fussi.

Naye Meneja wa Kituo cha Wwekezaji (TIC) Kanda ya Kati, Abubakar Ndwata, aliweka bayana fursa atakazopata mwekezaji atakayewekeza nchini.

"Tunawakaribisha wawekezaji kwani maeneo bado tunayo mengi. Waje wawekeze Manyoni," alisema Ndwata.

**"Kampuni hii iko tofauti na kampuni zingine kwasababu ikiuza korosho nje ya nchi, lile gawio la faida linarudi kwa mkulima na litamneemesha mkulima wa Singida," alisema Simbeye.**

## HABARI KITAIFA

# Mwangalizi afunguka siri ushindi CCM

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MMOJA wa waangalizi wa uchaguzi katika Jimbo la Kibaha, Prof. Benedict Mongula, amesema siri ya ushindi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni uwapo wa uongozi kuanzia ngazi ya shina hadi taifa.

Prof. Mongula ambaye ni mwanataaluma katika Taasisi ya Taaluma za Maendeleo (IDS) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salam, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa kuhusiana na mazingira aliyoshuhudia kipindi cha uchaguzi hadi matokeo yalipotangazwa.

Alisema amehudhuria mikutano ya kampeni kwa vyama vyote na kushuhudia maandalizi yalivyokuwa ambapo kulikuwa na tofauti kati ya CCM na vyama vingine vya siasa.

Kwa mujibu wa Prof. Mongula, ili vyama vya upinzani viwe imara, ni vizuri vikaanza kujiimarisha kuanzia ngazi ya shina kama ilivyo CCM.

Alisema katika mikutano ya CCM, maandalizi yalikuwa tofauti na mikutano mingine ya vyama vya siasa ambavyo baadhi ya mikutano ilikuwa haifanyiki.

"Nimefuatilia mazingira ya kampeni hadi wakati wa kupiga kura mpaka matokeo kutangazwa hali ilikuwa salama, hakukuwa na vurugu katika kipindi chote," alisema.

Alisema baadhi ya vyama vya upinzani walikuwa haviendi na ratiba kwa kuwa vilikuwa vikitangaza mikutano, lakini havifiki jambo ambalo kwenye maeneo hayo wananchi hawakupata fursa ya kusikia sera zao.

"Nafikiri na hali ya kifedha na maandalizi duni imechangia kampeni za vyama pinzani kudorora ingawa sina uhakika sana katika hili," alisema.

Alisema katika vituo alivyotembelea siku ya kupiga kura wapigakura walikuwa wachache na kwamba vituo vilifungwa kwa wakati ulipofika.

Kutokana na hali hiyo mwangalizi huyo alisema hata matokeo yalivyotangazwa hayakumshangaza.

# Wapatiwa mikopo ya milioni 117/-

**Na Mwandishi Wetu, BABATI**

MAKUNDI maalumu ya wanawake, vijana na wenye ulemavu katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, wamepatiwa mikopo isiyo na riba ya Sh. milioni 117.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, John Nchimbi, alisema jana kuwa halmashauri hiyo inaendelea kutekeleza sheria ya kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya makundi ya wanawake, walemavu na vijana.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha wa 2020/21, halmashauri hiyo imetenga Sh. milioni 241 ambapo vijana wamepatiwa Sh. milioni 96, wanawake Sh. milioni 96 na wenye ulemavu Sh. milioni 22.

Nchimbi alisema kwa mwaka wa fedha wa 2016/17 Halmashauri hiyo ilitoa mkopo wa thamani ya Sh. milioni 125 kwa vikundi 22 vya wanawake wakati vikundi tisa vya vijana vilipatiwa mkopo wa Sh. milioni 30.

"Kwa mwaka wa fedha wa 2017/18 Halmashauri ilitoa mkopo wa fedha wa Sh. milioni 155 kwa vikundi 26 vya wanawake vyenye jumla ya wanufaika 845 na vikundi vinane vya vijana vyenye wanufaika 40," alisema.

Alisema pamoja na kwamba mikopo hiyo haitakuwa na riba kama inayotolewa kwenye benki bado wanavikundi wanawajibika kurudisha mikopo hiyo kwa wakati ili makundi mengine yaendelee kunufaika.

"Hii mikopo haitolewi kama zawadi bali lengo lake ni kuwawezesha wasio na dhamana kama nyumba na viwanja kupata mikopo, tunatoa kwenye vikundi kwasababu tunaamini wakiwa kwenye vikundi wanaweza kusimamiana na wakairudisha kwa wakati," alisema Nchimbi.

Akikabidhi fedha hizo, Mkuu wa Wilaya ya Babati, Jacob Twange, aliwataka kuzitumia na kufanya yale waliyokusudia na kurudisha fedha hizo kwa wakati ili kuwapa fursa wengine wanaotaka mikopo hiyo.

"Hizi fedha zikitoka wananchi wanaamini kuwa ni fedha za serikali, ni kweli ni za serikali yenu na ndiyo maana imeamua kuwapa mikopo hii bila riba ili mkajiinue kiuchumi lakini lazima zirejeshwe ili wengine nao wapate," alisema Twange.

Alisema anaamini kuwa wakizisimamia vizuri fedha hizo zitawanufaisha na watazirejesha hivyo wasizitumie kwa anasa bali wakazifanyie kazi walizoombea.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

PONGEZI



Bodi ya Wakurugenzi, **Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka** ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), wanaungana na Watanzania wote kumpongeza Mheshimiwa, **Dkt. John Pombe Magufuli** kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

EWURA inapenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa itashiriki kikamilifu katika juhudi zake za mageuzi ya kiuchumi yenye lengo la kuinua maendeleo ya Taifa kwa **MATOKEO CHANYA.**

EWURA inamtakia Mheshimiwa Rais heri na fanaka katika utekelezaji wa ilani ya chama chake kwa manufaa ya Taifa.

*"UDHIBITI KWA MATOKEO CHANYA"*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la kheri JPM

LEO Rais Mteule wa Tanzania, Dk. John Magufuli, anaapa kumalizia muhula wa pili na wa mwisho wa kuiongoza serikali ya awamu ya tano, kwa mujibu wa Katiba.

Sherehe hizo zitafanyika katika Uwanja wa Jamuhuri, ikiwa ni mara ya kwanza kufanyika jijini Dodoma tangu serikali ilipohamishia ofisi zake zote pamoja na na taasisi zake.

Dk. Magufuli alishinda kwa kura zaidi ya milioni 12.5 sawa na asilimia 84.4, na kwa mujibu wa sheria za nchi Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ilimtangaza kuwa mshindi wa nafasi hiyo.

Kwa ushindi huo, tunampongeza na kumtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake kwa miaka mingine mitano.

Akizungumza Jumapili iliyopita wakati wa kukabidhiwa cheti cha ushindi kutoka NEC, alisema kwa ushindi huo aliopewa na Watanzania ni deni kubwa, ambalo litawafanya wafanyekazi usiku na mchana katika kuwatumikia Watanzania.

Wakati wa kampeni kila mgombea alikuwa na ilani yake, huku Chama Cha Mapinduzi (CCM), kikiwa na ilani ambayo wagombea wote waliinadi wakisema imebeba matumaini, matarajio ya Watanzania kwa miaka mingine mitano.

Aidha, vyama vingine vilivyosimamisha wagombea vilikuwa na ilani na katika kufanya kampeni vilikutana na wananchi wa maeneo mbalimbali, ambao walipaza sauti zao juu ya matatizo yanayowakabili katika maeneo yao. Kwa ujumla, baada ya kupata rais sasa ni wakati wa kutekeleza ilani na kuangalia masuala ya msingi ambayo yaliibuliwa na wagombea ubunge na udiwani kuyafanyia kazi, ili kuhakikisha kero za wananchi zinatatuliwa.

Katika miaka mitano, Dk. Magufuli alifanya kazi kubwa ya kuibua na kusimamia miradi ya maendeleo ambayo mingi imetekelezwa na kuleta mabadiliko makubwa kwa maisha ya watu, hususani miundombinu, ambayo imerahisisha usafiri kwa bidhaa, mazao na watu.

Pia, kazi kubwa imefanyika kwenye huduma za afya kwa kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Katika elimu, pia kazi kubwa imefanyika ikiwamo utoaji wa elimu bure, ambayo imewezesha wanafunzi wa familia zote kumudu gharama za masomo kirahisi kuanzia shule za msingi hadi kidato cha nne.

Sasa muda wa kumaliza kazi aliyoianza ni sasa baada ya kupata ridhaa ya Watanzania. Tunaamini ataangazia pia ilani za vyama vingine na kubeba yanayofaa kwa kuwa mwisho wa siku lengo lilikuwa ni kuwatumikia Watanzania wote. Watanzania ni vyema kutambua kuwa sasa uchaguzi umekwisha, na ni wakati wa kufanyakazi kwa bidii katika kujiletea maendeleo.

Hakuna muujiza wowote bila kufanya kazi, baada ya serikali kujenga mazingira wezeshi. Sasa ni wajibu wa kila mmoja kupigana eneo alilopo kuhakikisha anazalisha kipato cha familia yake na kujiwekea akiba.

Pia, ni muhimu tofauti za kiitikadi zikawekwa kando kwa kuwa sasa kinachozungumziwa siyo mchakato wa kura za maoni, kupiga kura wala kampeni bali ni wakati wa kuendelea na maisha baada ya uchaguzi. Ni ushauri wetu kuwa kusiwe na kubezana, kunyoosheana vidole, kuzodoana na kuwekana visasi kutokana tu na mtu kufanya maamuzi na kutumia uhuru na haki yake kikatiba kuonyesha upande au mgombea anayempenda.

Katika nchi ya kidemokrasia, maendeleo hayana itikadi, dini, rangi, kabila wala eneo analotoka mtu, na ili tubaki wamoja kama taifa, ni lazima kila mmoja akubali hali halisi na kusonga mbele.


Hakuna ubishi kuwa taifa lililo vipande vipande haliwezi kupiga hatua kimaendeleo, ni lazima kutibu majeraha ya uchaguzi ili kusonga mbele, vinginevyo ni kuendeleza maumivu ambayo hayataliponya taifa. Tanzania ni muhimu kuliko tofauti za kiitikadi, hivyo tuhatarajii kujenga ufa na utofauti wowote, bali kila mmoja awajibike kwa nafasi yake na kukubali uhalisia kwa kuwa ndiyo matakwa ya kikatiba.

Lakini tunaona ni muhimu sana katika kuliponya taifa kutafuta namna ya kuwa na maridhiano, ili kuondoa maumivu na namna yoyote ile ya malalamiko ambayo yalitokana na uchaguzi uliopita.

Tunasema kila la kheri Rais wetu, na tunakuombea utekelezaji mwema wa majukumu yake ya muhula wake ya mwisho wa serikali ya awamu ya tano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Lengo hili la maendeleo endelevu ni mwiba kwa ukatili wa kijinsia

Na Sabato Kasika

UKATILI wa kijinsia hususan kwa wanawake na watoto unaendelea na katika mwaka 2017 pekee, zaidi ya matukio 40,000 ya ukatili wa kijinsia yaliripotiwa, hali inayoonyesha bado vitendo hivyo vipo nchini.

Katika moja ya taarifa zake, aliyekuwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alihimiza na kuhimiza kila mdau kushiriki vita dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Dk. Ndugulile, mtaaluma wa tiba ya afya ya mwanadamu, pia mbunge mteule wa Kigamboni, anamtaka kila mdau kushiriki vita hivyo, kwa kuwa itasaidia kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's) ya Umoja wa Mataifa, hususan namba tano kuhusu usawa wa kijinsia, ifikapo mwaka 2030.

Suala la ukatili wa kijinsia dhidi ya makundi hayo, linatajwa kama ugonjwa unaoleta fedheha katika jamii zote na kwamba, likitajwa ni kinyume na maadili, pia kikwazo kwa maendeleo jumuishi yaliyo sawa na endelevu.

Vitendo vya ukatili vinaelezwa kudhihirisha ukosefu wa heshima, kushindwa kwa wanaume na ukatili kunaweza kuchukua sura yoyote, kuanzia nyumbani hadi usafirishaji haramu wa binadamu.

Mbali na hayo, ukatili mwingine unatajwa ni wa kingono hasa kwa ndoa za utotoni, ukeketaji, ambao kuna wakati unasababisha ama vifo au ulemavu wa kudumu kwa wanawake na wasichana, wakiwamo mabinti wadogo.

Kwa ujumla, ni aina ya ukatili unaowaumiza watu binafsi na kuathari familia na jamii kwa jumla, kwa kuwa unaambatana na mapana ya madaraka na udhibiti katika jamii.

Hivyo, umefika wakati sasa jamii ikabadilika na kuacha kuendelea kuishi katika mfumo hasi kama si dume, kwa sababu wanawake wanawekwa njia panda ya hatari ukatili, kupitia njia mbalimbali zinawakosesha usawa.

Ni wazi, uendelezaji mfumo huo ni kwenda kinyume na lengo Namba Tano la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDG's), linaloelekeza kutokomeza ukatili na ubaguzi dhidi ya wanawake na wasichana.

Lengo hilo linataka kuhakikisha wanawake wanapata fursa sawa katika umiliki wa rasilimali na nyanja zote za kimaisha, kwa kuwa ndio kundi lililonyimwa fursa kwa muda mrefu.

Pia kuna la kufanikisha lengo hilo ifikapo mwaka 2030, serikali za mitaa zinatakiwa kuondoa aina zote za ukatili na ubaguzi dhidi ya wanawake na wasichana, hata kugeuka mfano wa kuigwa katika kuleta usawa wa kijinsia.

Katika hilo, wanawake wanatakiwa kuwezeshwa kupata huduma za kijamii bila kubaguliwa, kupewa kipaumbele, kutambua na kutatua matendo hatarishi na ukatili unaowakabili.

Vilevile, huduma stahiki kwa walioathirika kwa ukatili huo ni muhimu, pia kuwapo kwa fursa za uongozi, umiliki ardhi utakaowezesha kuondoa mawazo mgando dhidi ya usawa wa kijinsia.

Muungwana anaamini kwamba, hayo na mengine mengi muhimu yakifanyika, kuna uwezekano mkubwa kutimiza lengo hilo na kuisaidia jamii ikaishi mbali na ukatili au ubaguzi wa aina yoyote.

Ikumbukwe kwamba, suala la ukatili wa kijinsia, ni kitendo chochote anachofanyiwa mtu kwa hali yake na kumwathiri kimwili, kiuchumi, kisaikolojia, kingono, bila kusahau pia ukatili wa mitandaoni.

Tanzania ina makabila mengi hivi sasa na kila moja lina utamaduni na mila zake, zikiwamo zilizopitwa na wakati. Yapo baadhi yanayoendeleza kukeketa, jamii zao zikiwa zimehamia mbali ikiwamo Jiji la Dar es Salaam na kuendeleza mila hizo, makabila hayo ni vyema yakafuatiliwa na kuchukuliwa hatua, ili kukomesha ukatili ulivyo.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto katika Makao Makuu ya Polisi, Faidha Suleiman, amewahi kuthibitisha hayo katika semina moja jijini Dar es Salaam na kutaja maeneo yenyewe kuwa Kitunda.

Hivyo, kampeni na ufadhili unatolewa kwa ajili ya kupambana na ukatili huo, vizae matunda, hasa kwa jamii yenyewe kubadilika na kutambua kuwa mila hizo zimeshapitwa na wakati, si za kuendekeza tena.

Inasikitisha kuendelea kuona, jamii iliyogubikwa na matukio ya ukatili wa kijinsia inafanya hivyo. Ni hatari, pia iko na lengo tajwa la SDG.

HABARI KITAIFA

# Mtuhumiwa kesi mauaji aachiwa huru

**Na Said Hamdani, LINDI.**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Mtwara imemwachia huru mkazi wa Kijiji cha Muungurumo, Wilaya ya Liwale, Lindi, Ally Mwinyanda, maarufu kama Masharubu, baada ya upande wa mashtaka kushindwa kupeleka ushashidi ambao ungemtia hatiani.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Jaji Wilbrod Dyansobera, baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha kosa.

Kabla ya kutolewa kwa uamuzi huo, Wakili Robert Dadaya, aliyekuwa akimtetea Masharubu, aliiomba mahakama kumwachia huru mteja wake kutokana na upande wa Jamhuri kushindwa kuwasilisha ushahidi ambao ungeisaidia mahakama kutenda Haki.

Wakili Dadaya alidai kutokana na mteja wake kukaa ndani kwa kipindi kirefu, upande wa mashtaka ulikuwa na nafasi ya kuhakikisha wanaupata na kuwasilisha mbele ya mahakama hiyo.

Jaji Dyasonbera, akitoa uamuzi katika kesi hiyo, alisema kutokana na upande wa mashtaka kushindwa kuwasilisha ushahidi wa kutosheleza ambao ungesaidia kumtia mshtakiwa hatiani, anamwachia huru chini ya kifungu 312 (3) cha Sheria ya Mwendendo wa Mashtaka (CPA).

Awali, ilidaiwa mbele ya mahakama hiyo na Mwanasheria wa Serikali Emmanuel John, kuwa Julai 19/2016 usiku, Masharubu alimuua Athumani Chitawala wa Kijiji cha Mungurumo, Wilaya ya Liwale, Mkoani Lindi.

Mwanasheria huyo alidai kuwa siku ya tukio, Masharubu alifika nyumbani kwa Chitawala na kumkuta akiwa na mwenzake ambaye ni mlemavu wa macho akiota moto na kuchomoa kisu na kumkata tumboni kisha kufariki dunia.



Mafundi wakiwa kwenye maandalizi ya mwisho ya matengenezo ya jukwaa katika uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana, litakalotumika kumwapisha Rais Mteule Dk. John Magufuli, leo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RC Lindi aonya kuhusu ugaidi

**Na Said Hamdani, LINDI**

SERIKALI mkoani Lindi, imewataka wananchi kutokubali kupokea watu wasiowafahamu wanaofika katika maeneo yao ili kulinda usalama wa maisha yao na taifa kwa ujumla.

Tahadhari hiyo ya serikali imetolewa kutokana na taarifa za uwapo wa magaidi katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari mjini hapa.

Zambi ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Lindi, alisema hali ni tete mpakani mwa nchi hizo mbili kutokana na watu wanaodaiwa kuwa magaidi kuingia na kuweka kambi.

"Hali ni mbaya kaskazini ya Msumbiji na kusini mwa nchi yetu, hivyo kama mkoa na kanda yetu ya kusini, tumeanza kupata athari za uwapo wa watu hao," alisema Zambi.

Kwa mujibu wa Zambi, tayari kuna watu wameanza kuingia maeneo mbalimbali ya Lindi kwa sura ya kufanya biashara, kuendesha masuala ya dini na kusalimia ndugu na jamaa zao, na kwamba hiyo inaweza kuwa njia ya kuwa na nia ovu ya kufanya uhalifu.

Zambi alisema katika mkoa wa Lindi wameshakutana na makundi ya watu mbalimbali, huku akiwasisitiza wamiliki wa nyumba za kulala wageni kuwa makini na watu wanaofika kuhitaji huduma za malazi.

Pia kiongozi huyo alizitaka kamati za ulinzi na usalama kuanzia ngazi za vitongoji, kuhakikisha zinaweka mikakati itakayosaidia kuimarisha ulinzi huku akiwaomba waandishi kupitia vyombo wanavyovitumikia kuelimisha jamii kuhusiana masuala yanayoendelea hivi sasa.

Sambamba na hilo, aliwasisitiza wazazi na walezi kuhakikisha wanawachunga vijana wao wanaosoma shule zilizo mbali na maeneo yao kwenda na kurejea nyumbani ili wasije wakatekwa kama ilivyokuwa katika mataifa mengine.




# Lukuvi apokea taarifa ya awali ya uhakiki mgogoro

**Na Munir Shemweta, DODOMA**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi (pichani), amepokea taarifa ya awali ya uhakiki wa eneo la Mtakuja lenye mgogoro lililoko katika Kata ya Chang'ombe, jijini Dodoma.

Taarifa ya uhakiki wa eneo hilo lenye ukubwa hekta 10, iliwasilishwa jana katika ofisi za wizara, Mtumba jijini hapa na Kamishna Msaidizi wa Ardhi Uratibu, Wilson Luge, kwa niaba ya timu inayofanya uhakiki kwa wakazi wanaoishi eneo hilo.

Uwasilishaji taarifa hiyo unatokana na kukwama kwa mara kadhaa kwa uhakiki uliofanyika mara kadhaa hapo awali na kusababisha Waziri Lukuvi kuelekeza kufanyika uhakiki mwingine ili kutafuta suluhu ya kudumu ya mgogoro huo.

Kwa mujibu wa Luge, tayari timu ya uhakiki mgogoro huo imeshawapitia



wananchi 750 kati ya 1,025 watakaofanyiwa uhakiki.

Luge alisema kazi kubwa inayofanywa na timu ya uhakiki ni kupitia taarifa ya kila mwananchi na kuangalia hali ya maendelezo yaliyofanyika katika kila eneo analomiliki.

Uhakiki eneo la Mtakuja umefanyika mara kadhaa mwaka 2005, 2008 na 2015 ambapo kazi inayoendelea sasa inatarajiwa kuleta suluhu ya mgogoro huo.

Uwasilishwaji taarifa ya uhakiki wa mgogoro huo ulihudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira ambaye ni Mbunge Mteule wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mary Makondo, Naibu wake Nocholaus Mkapa, Kamishna wa Ardhi, Nathaniel Nhonge, na watendaji wa wizara, Jiji la Dodoma wa Kata ya Chang'ombe.

# Wadau elimu wafurahia ushindi wa JPM

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa elimu nchini wamempongeza Rais John Magufuli kutokana na ushindi mkubwa alioupata kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Mkuu wa Shule ya Hazina ya jijini Dar es Salaam, Omari Juma, alisema jana kuwa wamefurahishwa na ushindi wa Rais Magufuli kwa kuwa serikali yake imekuwa msaada mkubwa wa wadau wa elimu wa sekta binafsi.

Alisema ushindi huo umedhihirisha namna Watanzania wanavyomkubali kutokana na utendaji kazi wake uliotukuka na namna alivyoiinua sekta ya elimu nchini.

Alisema Rais Magufuli tangu aingie madarakani Novemba, 2015 ameifanyia nchi mambo makubwa hali ambayo imeongeza imani kwa wananchi kuwa ni kiongozi bora hivyo kumchagua kwa kura nyingi ili aongoze kwa muhula mwingine.

"Sisi wadau wa elimu wa sekta binafsi tumefurahishwa sana na ushindi wa kishindo wa Rais Magufuli kwa sababu serikali ya awamu ya tano imetufanyia mengi mazuri na imekuwa ikitoa ushirikiano sana kwa sekta binafsi upande wa elimu," alisema.

Alisema wana imani kubwa na Rais Magufuli kwamba licha ya kuiendeleza nchi kimiundombinu serikali yake itaendelea kushirikiana na sekta binafsi upande wa elimu.


Eliezer Semfuko, ambaye ni mmiliki wa shule ya Sunray, alisema sekta ya elimu imefanya vizuri katika awamu ya tano ya Rais Magufuli hivyo ushindi wake ni ushindi kwa sekta ya elimu.

Alisema Rais Magufuli ameipa kipaumbele sekta ya elimu kwa kutoa elimu bure kwa watoto wa Watanzania na kuhakikisha sekta hiyo inazidi kukua siku hadi siku kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mdau mwingine wa elimu kutoka shule ya msingi Precious ya Mbagala, John Mapunda, alisema sekta binafsi upande wa elimu wanamengi ya kujivunia kutokana na uongozi mahiri wa Rais Magufuli.

"Kwa upande wa elimu amefanya mengi makubwa ambayo tunaamini kwa kupewa miaka mingine mitano ataendeleza yale mazuri tuliyoyapata awamu iliyopita tunaomba sekta binafsi na ya umma tuendelee kushikamana maana wote tunajenga nyumba moja," alisema Mapunda.

Rais Magufuli anaapishwa leo mkoani Dodoma baada ya kushinda kwa kishindo kwa kupata kura milioni 12.5 kwenye uchaguzi uliopita huku anayefuata akipata kura milioni 1.9.



Bibi kizee akitafuta chupa tupu za plastiki katika eneo la Mikocheni, jijini Dar es Salaam hivi karibuni, kwa ajili ya kwenda kuziuza ili kujipatia riziki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TARURA ilivyoboresha barabara za Newala

**Na Bebi Kapenya**

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) katika Halmashauri ya Mji wa Newala mkoani Mtwara, umeendelea kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji kwa kujenga miundombinu ya barabara na vivuko katika maeneo mbalimbali wilayani humo.

Meneja wa TARURA Halmashauri ya Mji wa Newala, Mhandisi Dickson Mkokota, alisema, ujenzi wa Barabara ya Kiduni-Makondeko - Mkunya kwa kiwango cha Lami yenye urefu wa kilomita 1 utasaidia kurahisisha usafiri na kufikia kwa urahisi huduma za kijamii kwa sababu barabara hiyo ni njia inayoelekea moja kwa moja kwenye chanzo kikuu cha maji yanayotumiwa na wananchi wote wa Newala.

"Ujenzi wa barabara hii utagharimu zaidi ya shilingi milioni 400, barabara itakuwa na mifereji ya kukusanya maji, makaravati na vivuko vidogo vinavyoingia kwenye mitaa hasa maeneo ya nyumba za ibada, ili kurahisisha usafiri kwa wananchi wa eneo hili waweze kusafirisha mazao yao kwa urahisi," alisema Meneja huyo.

Naye Shekhe Mpota, mkazi wa Newala, aliishukuru serikali kwa ujenzi wa barabara hiyo itakayoleta unafuu mkubwa kwa wananchi ambayo itapelekea kusafirisha mazao yao kwa urahisi ikiwamo korosho, mbaazi na ufuta.

"Tunaishukuru serikali kwa ujenzi wa barabara hii kwa sababu itatuondolea kero ya kusafirisha mazao yetu hasa korosho kwa vile korosho zote za Newala Mjini zinatoka mashambani…barabara hii inaelekea na kuja huku mjini, hivyo ikikamilika itatusaidia sana kusafirisha mazao yetu na kufanya biashara kwa urahisi," alisema.

Kadhalika alisema kwamba ni njia rahisi ya kufika mpakani mwa Msumbiji kwa kupitia Mto Ruvuma.

Mbali na utekelezaji wa mradi huo, TARURA katika Halmashauri ya Mji wa Newala imekamilisha ujenzi wa Barabara ya Elimu kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita moja katika eneo la Nangwala, imefanya matengenezo ya barabara za Newala mjini kwa kuchonga barabara kwenye makazi ya wananchi eneo la PCCB Km 16 ambazo zimeshakamilika na imekamilisha ujenzi wa korongo eneo la Julia lenye urefu wa mita 150 na upana usiopungua mita tatu.

Kwa mujibu wa meneja huyo, korongo hilo limesaidia kupunguza kero kwa wananchi kutokana na maji ya mvua yaliyokuwa yanaathiri makazi ya watu na mashamba.

TARURA) katika Halmashauri ya Mji wa Newala inahudumia mtandao wa barabara wenye urefu wa kilomita 406, na jitihada za uboreshaji wa huduma za usafiri na usafirishaji ili kuinua uchumi wa wananchi.

## HABARI KITAIFA

# Mgombea ubunge kwenda kortini

**Na Said Hamdani,** LINDI

ALIYEKUWA mgombea ubunge Jimbo la Lindi Mjini kupitia ACT-Wazalendo, Isihaka Mchinjita, anajiandaa kwenda mahakamani kufungua kesi kupinga ushindi aliopewa Hamida Abdallah wa CCM, uliotangazwa na msimamizi wa uchaguzi, Jomaari Satura, kwa madai uligubikwa na hujuma nyingi.

Mchinjita ameyaeleza hayo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa mjini Lindi, na kwamba ameamua kuchukua hatua hiyo baada ya kubaini kuwapo kwa hujuma na kasoro mbalimbali wakati wote wa upigaji kura Oktoba 28, mwaka huu.

Mchinjita ametaja baadhi ya hujuma zinazodaiwa kufanyika ni baadhi ya mawakala wao kukataliwa kuingia vituo vya kupigia kura, licha ya kuapishwa kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Alitaja kasoro zingine ni baadhi ya watu kukamatwa wakiwa na kura, ongezeko la vituo hewa vilivyo nje ya mfumo, kubadilishiwa matokeo na ucheleweshwaji wa kutoa matokeo.

"Wapo watu tumewakamata wakiwa na kura akiwemo muuguzi mmoja (jina limehifadhiwa), akiwa na katarasi sita, tukamfikisha Kituo cha Polisi, alipoulizwa alikiri na kueleza wapo wengi waliopewa," alisema Mchinjita.

Mchinjita alisema licha ya mama huyo kufikishwa kituo cha Polisi, aliachiwa huru na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi yake. Katika uchaguzi wa madiwani, wabunge na Rais, mgombea ubunge wa Jimbo la Lindi Mjini, Hamida Abdallah Mohamedi (CCM) alitangazwa mshindi.



Ofisa wa Benki ya NMB, Julieth Kishamba, akitoa maelekezo kwa wafanyabiashara wa wilayani Kasulu, jinsi ya kujaza fomu za mikopo na maelezo ya biashara zao, wilayani humo, mkoani Kigoma. Benki hiyo, iliwakutanisha zaidi ya wafanyabiashara 200 mkoa huo, ili kuwapa elimu ya fedha na bidhaa mbalimbali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge wa zamani CUF awapa somo wapinzani

**Na Thobias Mwanakatwe**

MBUNGE mstaafu wa Chama cha Wananchi (CUF) Jimbo la Kigamboni, Frank Magoba, amevitaka vyama vya upinzani kuacha kulalamika na kuandaa maandamano kwa kuwa kushindwa kwao kwenye uchaguzi wa mwaka huu kunatokana na wao kushindwa kuungana na kuunda chama kimoja chenye nguvu kinachoweza kuing'oa CCM madarakani.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu ambao Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeibuka na ushindi mkubwa.

Magoba alisema wakati akiwa CUF alikuwa akishauri mara kadhaa kwamba kama vyama vya upinzani vinadhamira ya kweli ya kutaka kuing'oa CCM madarakani vinatakiwa viungane pamoja na kuunda chama kimoja chenye nguvu, lakini kuacha kila chama kuweka mgombea wake wa urais, ubunge na udiwani kamwe CCM haitakuja kung'olewa.

Alisema jambo jingine ambalo limesababisha wananchi wasivichague vyama vya upinzani katika uchaguzi wa mwaka huu ni kauli zisizokuwa na ustaarabu ambazo zilikuwa zikitolewa na baadhi ya wagombea.

"Watanzania wa leo sio wa mwaka ule, wana uelewa sana, wewe mgombea unapoanza kuzungumzia matusi na kebehi kwa serikali wakati wanaona kuna maendeleo yamefanywa na serikali hiyo unayoitukana hawezi kukuelewa," alisema.

Magoba aliongeza kuwa utendaji mzuri wa Rais Dk. John Magufuli ndio umeteka mioyo ya Watanzania ambao wameamua kumchagua kwa miaka mingine mitano.

Hata hivyo, alisema yapo baadhi ya mambo ambayo Rais Magufuli anapaswa kuyatupia mambo kipindi hiki ambayo ni ukosefu wa dawa katika hospitali, wazee kutotibiwa bure katika baadhi ya hospitali, tatizo la maji, upungufu wa vyumba vya madarasa na migogoro ya ardhi ambayo bado rushwa inatumika.

Alivipongeza vyama vya upinzani kwa kushiriki uchaguzi mkuu kwa kupiga kampeni bila kuchoka na kwamba kushindwa kwao wasikate tamaa bali wajipange kwa ajili ya uchaguzi ujao.


PASS
PRIVATE AGRICULTURAL SECTOR SUPPORT

## CONSULTANCY ON COMMISSIONING A CALL CENTRE
## TERMS OF REFERENCE

**Background on PASS Trust**
The Private Agricultural Sector Support (PASS) Trust was established as the project in year 2000 in order to stimulate investments and growth in private sector commercial agriculture and related sector through access to finance in Tanzania. It was registered in 2007 as an autonomous non-profit organization under the Trustees' Incorporation Act of Tanzania, founded by Government of Denmark and Government of Tanzania.

For many years access to finance for the agricultural sector has been challenging in Africa, and Tanzania in particular. Financial Service Providers (FSP), mainly Banks, have viewed it as too risky to finance due to, among other reasons, weak collateral, poor production skills, low technical skills and a general lack of bankable investment opportunities which would provide FSPs with a commercial incentive to finance. PASS Trust has a vision to unlock this challenge and aspiring to be an innovative agri-finance development institution that improves the quality of life for small-scale agribusiness entrepreneurs. Its mission is to facilitate access to financial and business development services for agribusiness entrepreneurs in Tanzania.

**Objective of the Consultancy**
PASS Trust has an existing telephony system (VOIP System) which acts a communication channel within the organization. This happened due to PASS vision of transforming its operations to digital. The system supports all PASS Trust offices including Arusha, Dar es Salaam, kigoma, Mbeya, Morogoro, Mwanza and Mtwara. To increase outreach and efficiency PASS Trust is about to implement a robust call centre through a toll-free line that will allow stakeholders to engage with PASS Trust for information, support and awareness to PASS Trust products.

The new call centre system is expected to integrate with the existing VOIP System which will enable customer agents to route of calls to PASS extensions. To build the state-of-the-art call centre the following initiatives will be considered:

1. To ensure efficiency in service delivery through effective communication, learning and sharing of information as envisaged in our 2018-2022 strategic plan.
2. To ensure more Tanzanians are facilitated towards accessing financial and business services- mainly small and medium size commercial farmers, farmer groups and agribusinesses (SMEs).
3. To improve our customer experience and engagement with our stakeholders.

Therefore, PASS intends to engage an experienced vendor who has experience in call centre deployment for in-house customer service.

**Scope of Work**
Under the supervision of ICT unit, the vendor shall perform the following tasks:

1. Work with ICT Unit and Communication specialist on gathering of information that will define the call centre architecture, workflows and functional requirements for call centre call reports requirements.
2. Install the call centre that will be able to work with Softphone in Windows Environment and VOIP handsets.
3. Integrate the call centre to the existing PASS Trust Yeastar S100 VOIP PBX
4. Train PASS Call Centre Staff

**Requirements and Deliverables**

- **Language**
  The vendor shall ensure that English and Swahili are properly set up to manage both languages. The system should let the customer agent know the preferred language of the caller.

- **Interactive Voice Response (IVR)**
  The vendor shall ensure that the IVR feature is set up on the system based on the PASS requirements. The IVR shall provide the caller the ability to:
  a) Select one of the two languages either English or Swahili
  b) Listen to pre-recorded information
  c) Ask the caller to use the touch-tones and guide the caller to an area of interest

- **Call Recordings**
  a) The vendor shall ensure the system in place is set up to record all the voicemails, calls, call-backs made and calls received by PASS. All call recordings shall be stored on a storage that can be easily retrieved.
  b) The vendor shall ensure that the system informs all callers that their calls are recorded or monitored.

- **Call Queues**
  The vendor shall ensure the system is set up for call queuing. When a caller finish going through the Interactive Voice Response (IVR) prompts and unable to reach to get a customer agent. The system should place the caller on the queue waiting for a customer agent to free up.

- **Call Transfer**
  The vendor shall ensure that the system is set up for a customer agent to be able to transfer calls without disconnecting the caller. Calls can be transferred to another customer agent of can be transferred to PASS VOIP system to the intended extension.

- **System Monitoring and Reports**

a) The vendor shall ensure that the system provides PASS with a real-time dashboard for monitoring call activities. The dashboard shall display real-time status of call statistics including and not limited to the following:
  - Number of agents on calls
  - Number of agents online
  - Number of agents offline
  - Calls in queue for each agent
  - Calls abandoned
  - Calls answered
  - Longest call on wait in the queue
  - Average wait time

b) **Regular Reports**
  The system shall be able to report various reports including but not limited to the following:
  - Generate reports of different PASS Products based on the incoming calls
  - Generate reports on how many Calls have been abandoned
  - Generate reports on how many Calls have been answered
  - Generate reports on the Longest call on wait in the queue
  - Generate reports on Average wait time
  - Generate reports on how long customer agent has been online
  - Generate reports on how many calls customer agent has received

- **Training**
  The vendor shall train PASS Customer Agents and ICT Unit. The training shall ensure the customer agents are equipped with the proper knowledge and skills in handling the calls and support the system.

- **Provisional of the Operational Manual of the System**
  The vendor shall produce operational manual for customer agents, administrators and including but not limited to troubleshooting of simple system errors.

**Qualifications and Experience:**
The ideal vendor must have relevant qualifications which include but not limited to

- Proven expertise in deployment of call centre include list of certified engineers and Manufacturer Authorization letter.
- Must have experience in deployment of call center platforms with at least three references of similar project.
- Must have all business legal documents/Certificates (TIN, VRN, Business License, TCRA, Certificate of Incorporation)

Interested vendors will be required to submit their Technical and Financial Proposals electronically as per this TOR Guidelines to the web address: **https://pass.or.tz/procurement** and click the APPLY NOW button to upload and submit your proposal. Unfortunately, due to the large volume of proposals we receive, we will not be able to respond to each individual proposal/bidder, only the shortlisted/awarded bidders will be contacted. As PASS Trust commitment to Inclusive Green Growth (IGG) strategy and paperless office, we will only accept electronic submissions and not physical submission. The deadline to receive the proposals shall be on **16th November 2020, 12.00 noon.**

HABARI KITAIFA

# Wakamatwa hifadhi ya taifa wakidaiwa wahamiaji haramu

**Na Thobias Mwanakatwe**

JESHI la Uhifadhi na Misitu Kikosi cha Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) linawashikilia raia 49 wa Ethiopia katika Hifadhi ya Taifa ya Saadani.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi na Mawasiliano, Pascal Shelutete, alisema watu hao walikamatwa juzi katika Kijiji cha Saadan kando ya Bahari ya Hindi Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani.

**Watu hao walikamatwa juzi katika Kijiji cha Saadan kando ya Bahari ya Hindi Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani.**

Alisema kukamatwa kwa watuhumiwa kumetokana na ushirikiano mkubwa walioupata kutoka kwa wananchi wa kijiji hicho na kwamba uongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Saadani umewakabidhi wahamiaji hao kwa Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji kwa hatua zaidi za kisheria.

Shelutete alisema TANAPA inaendelea kusisitiza na kutoa onyo kwa wale wenye dhamira ya kutumia Hifadhi za Taifa kwa vitendo ambavyo ni kinyume na sheria kuacha mara moja kwani wakibainika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Jeshi la Uhifadhi na Misitu limejipanga vyema kuhakikisha kuwa maeneo ya hifadhi yanaendelea kuwa salama kwa shughuli za hifadhi na utalii na si vinginevyo," alisema.

Aidha, amewaomba wananchi wanaozunguka hifadhi za taifa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Uhifadhi na Misitu kwa kuwafichua watu wanaotaka kufanya vitendo viovu katika hifadhi ili waweze kuchukuliwa hatua.



Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel (katikati), Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Richard Jordinson (kushoto) na Meneja Uhusiano wa GGML, Joseph Mangilima, wakiteta jambo baada ya uzinduzi wa ujenzi wa bustani ya kisasa katikati ya mji wa Geita jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# GGML yaanzisha bustani ya kuvutia Geita

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa mji wa Geita wanafurahia kuwa sehemu ya mradi wa bustani ya kupumzikia inayofadhiliwa na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji Geita.

Mradi huo uliotengewa bajeti ya Sh. milioni 70 kutoka fedha za GGML za uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR) zinatarajiwa kukamilisha mradi huo kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Akizungumza katika hafla ya kuzindua ujenzi wa bustani hiyo katika kata ya Kalangalala mjini Geita, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel, alisema GGML kwa kushirikiana na Halmashauri ya Geita Mji inatekeleza mradi huo kupitia fedha za CSR kutoka GGML.

Mradi huo unaotekelezwa katika eneo la mita za mraba 4,000 katika kata ya Kalangalala mjini Geita, una lengo la kuwapatia wakazi wa Mji wa Geita fursa ya kuwa na eneo la kufanya shughuli mbalimbali zikiwamo kupumzika, kupunga upepo pamoja na kuepuka kero za joto.

"Lengo letu ni kuona wakazi wa Mji wa Geita wanafika katika eneo hili kufurahia upepo asilia sambamba na kuona mnara maalum wenye kumbukumbu ya Mkoa wa Geita. Bustani hii itakuwa kivutio pia kwa vile inajengwa kwa tofali za kuvutia kwenye maeneo yote ya kupitia na sehemu za watu kuketi hali ambayo itashawishi watu wengi zaidi kukaa na kujionea uzuri wa Mji wetu wa Geita," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Richard Jordinson, alisema kuwa Kampuni ya GGML imekuwa ikifanya jitihada kubwa kubadilisha mwonekano wa jamii ya Mkoa wa Geita kwa kuanzisha miradi endelevu.

"GGML tunajivunia kuwa, wakati tunasherehekea miaka 20 ya uwekezaji wetu ndani ya Mkoa wa Geita mwaka huu, tumefanikiwa kutekeleza miradi mingi yenye tija na matokeo chanya ikiwemo mnara wa makutano ya barabara Mjini Geita, masoko, taa za barabarani, vituo vya afya, shule na barabara za lami," alisema Jordinson.

# Mwangalizi atoa tathmini uchaguzi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MMOJA wa waangalizi wa uchaguzi katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Prof. Benedict Mongula, amesema siri ya ushindi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni uwapo wa uongozi kuanzia ngazi ya shina hadi taifa.

Prof. Mongula ambaye ni Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salam, alisema alihudhuria katika mikutano ya kampeni ya vyama vyote na kushuhudia maandalizi yaliyokuwa, na kwamba kulikuwa na utofauti kwa CCM na vyama vingine vya siasa.

Alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari Mjini Kibaha, kuhusiana na mazingira aliyoshuhudia kipindi cha uchaguzi hadi matokeo yalipotangazwa.

Alisema ili vyama vya siasa vya upinzani viwe imara, ni vizuri wakaanza kujiimarisha kuanzia ngazi ya shina kama ilivyo CCM.

Alisema katika mikutano ya CCM maandalizi yalikuwa tofauti na mikutano mingine ya vyama vya siasa vya upinzani, ambavyo baadhi ya mikutano haikufanyika.

"Nimefuatilia mazingira ya kampeni hadi wakati wa kupiga kura mpaka matokeo kutangazwa...hali ilikuwa salama, hakukuwa na vurugu katika kipindi chote," alisema.

Alisema baadhi ya vyama vya upinzani walikuwa hawaendi na ratiba, kwani walikuwa wakitangaza mikutano, lakini hawafiki, jambo ambalo kwenye maeneo hayo wananchi hawakupata fursa ya kusikia sera zao.

"Nafikiri na hali ya kifedha na maandalizi duni imechangia kampeni za vyama vya upinzani kudorora, ingawa sina uhakika sana katika hili," alisema.

Alisema katika vituo alivyotembelea siku ya kupiga kura, wapigakura walikuwa wachache na kwamba vituo vilifungwa kwa wakati muda ulipofika.

**Baadhi ya vyama vya upinzani walikuwa hawaendi na ratiba, kwani walikuwa wakitangaza mikutano, lakini hawafiki, jambo ambalo kwenye maeneo hayo wananchi hawakupata fursa ya kusikia sera zao.**


# ama

ALHAMISI NOVEMBA 5, 2020 AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

## Msuguano wafugaji na wasimamizi hifadhi katika maisha ya kuogopana



Ukurasa 13

## Mabadiliko ya tabianchi yalivyo chanzo kubomoka madaraja Moro

# Wimbi jipya maradhi corona lazusha taharuki bara Ulaya

**Na Rashid Chilumba**

HASIRA na wasiwasi zinaongezeka miongoni mwa wakazi wa mataifa mengi barani Ulaya, kutokana na kurejea tena vizuizi vikali vya kukabiliana na maambukizi pamoja na vifo vitokanavyo na maradhi ya COVID-19.

Katika kile kinachoonekana kuwa ishara za kukata tamaa, waandamanaji kwenye miji kadhaa nchini Hispania, mwishoni mwa wiki walipambana na vikosi vya usalama kupinga kurejeshwa kwa marufuku ya shughuli za kawaida kujaribu kupambana na kitisho cha virusi vya maardhi ya corona.

Hivi sasa nchini Hispania, kunatekelezwa amri ya kutotoka nje usiku na karibu majimbo yote ya nchi yameifunga mipaka ya ndani kuzuia safari za masafa marefu.

Serikali ndani ya Bara Ulaya, zinahangaika kupunguza ongezeko la kutisha la maambukizi ya virusi vya corona, ambayo hadi sasa yamesababisha vifo vya watu 279,000 barani humo tangu vilipozuka nchini China mwishoni mwa mwaka jana.

Nchini Uingereza, wengi wanaelezea wasiwasi walio nao kuhusu hasara ya kiuchumi itakayopatikana katika muda wa wiki nne, ambao shughuli zote za kawaida zitafungwa.

Huko Italia ambako kumeshuhudiwa maandamano makubwa wiki iliyopita, serikali inatarajiwa kutangaza hatua mpya za vizuizi baadaye hivi leo.

Inaarifiwa kuwa, serikali inalenga kupiga marufuku safari kati ya jimbo moja na jingine, kufunga maduka makubwa, kupunguza shughuli za biashara na kuzuia watu kutoka nje usiku.



Corona ni shida kubwa. Ndivyo ilivyokuwa kampeni ya kuikabili mitaani, janga lililofanikiwa kuzimwa nchini. **PICHA: MAKTABA.**

Mjini Munich, Ujerumani, maeneo ambayo kwa kawaida hufurika watu, hivi sasa yako tupu na nchi hiyop imeshaanza Jumanne iliyopita, kutekeleza awamu mpya ya vizuizi ikiwa ni pamoja na marufuku ya mikusanyiko, kufungwa kumbi za starehe na maduka yasiyo na bidhaa zinazohitajika kwa wingi, pamoja na kuwaisitiza watu kuvaa barakoa.

> **Inafaa kusahau mwaka huu mzima. Kabla ya marufuku ya kwanza, mwezi Februari, hakukuwa na cha kuingiza kwa sababu kila kitu kilishindana. Hata msimu wa kiangazi, ambako kwa baadhi ya wakati bustani zilijaa watu, ilikuwa ni sawa na tone kwenye bahari.**

Meneja wa mgahawa uliopo nchini Ujerumani, anayejitambulisha kwa jina la Christian Lehner, ana maoni yake: "Athari za kiuchumi wala hazipimiki tena, mwaka huu wote unapaswa kusahaulika.

"Inafaa kusahau mwaka huu mzima. Kabla ya marufuku ya kwanza, mwezi Februari, hakukuwa na cha kuingiza kwa sababu kila kitu kilishindana. Hata msimu wa kiangazi, ambako kwa baadhi ya wakati bustani zilijaa watu, ilikuwa ni sawa na tone kwenye bahari.

"Sasa tunaingiza sehemu tu ya kile tunachohitaji kuishi. Mwaka huu siyo wa kutengeneza tena pesa. Ni mwaka wa kujiokoa tu kiuchumi, kulinda ajira na kampuni."

"Kwingineko waziri mkuu wa Ufaransa Jean Castex amesema kuanzia (juzi) Jumanne maduka makubwa yatapigwa mafuruku kuuza bidhaa ´zisizo muhimu´ kama ilivyokuwa kwa wauzaji wadogo waliolazimika kufunga maduka yao."

**BOSI NAYE**

Mkurugenzi Mkuu Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Tedros Ghebreyesus, anasema kwamba anasema anajiweka karantini baada ya kukutana na mtu ambaye sasa amebainika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona.

Katika ukurasa wake wa mtandao wa Twitter, Tedros anaesema, bado ana afya njema bila dalili za COVID-19, lakini atasalia karantini kwa siku kadhaa zinazokuja kama taratibu za WHO zinavyoelekeza.

Tedros anasema ni muhimu kuzingatia miongozo ya wataalamu wa afya kwa lengo la kudhibiti kusambaa kwa virusi vya corona na kuikinga mifumo ya afya kutozidiwa na idadi ya wagonjwa.

Wiki iliyopita mkurugenzi huyo wa WHO, aliwatolea wito viongozi wa dunia kuzingatia ushauri wa wataalamu katika wakati idadi ya maambukizi inapanda barani Ulaya na kwenye mataifa ya Amerika Kaskazini.

*DW*

MAZINGIRA

WAKATI UHARIBIFU UNAENDELEA...

# Msuguano wafugaji na wasimamizi hifadhi katika maisha ya kuogopana

## •Kilio cha elimu duni kila kona
## •DC Mbarali aibua ya uvunguni

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa Mbarali**

BADO kuna elimu duni, hali ya kuogopana kati ya wasimamizi wa wanyamapori na wanavijiji jirani. Shida kuu, hata wanavijiji wawaogopa askari wanyamapori, inatajwa elimu duni katika dhana ya kinachoendelea mahali hapo.

Hatima ya yote ni kuwapo migogoro isiyo ya lazima ndani ya jamii. Leo hii dhana kuu inayotawala ni wakazi wa vijiji jirani na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha Kanda ya Kusini, wanaomba kupatiwa elimu sahihi kuhusu uhifadhi na wanyamapori, itakayomaliza migogoro kati ya pande hizo mbili.

Ni salamu zinazotoka kwa baadhi ya vijiji kama vile Igava, Vikawe, Igunda, Mawindi na Iwalanje vinavyoeleza kukabiliwa na uhaba wa elimu na wananchi kujikuta wakiwakimbia wanaohusika na hifadhi, hata kama hawajafanya makosa.

Ofisa Mtendaji wa Kitongoji cha Mawindi, Edson Kilemile, anasema licha ya kuwapo faida za kuwa karibu na hifadhi, bado elimu duni kuhusu uhifadhi wa wanyamapori ni tatizo, hata kuna migogoro isiyo ya lazima.

Kilemuile anasema, wapo wananchi ambao inapotokea wanawaona askari a wanyamapori, basi wanawakimbia, licha ya kwamba hawajafanya uhalifu wowote.

"Kitendo cha kuwakimbia watu wa hifadhi kimekuwa kikizua taharuki na wakati mwingine kusababisha kukamatwa kwa kudhaniwa ni wahalifu," anasema, huku akihimiza elimu sahihi itakayowakomboa kutoka kwenye adha hiyo.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mawindi, Hamo Gaudai, anasema kutokana na tatizo hilo, anaiomba taasisi husika kutoa elimu kwa kutembelea kila kijiji kuhakikisha wananchi wanaozunguka hifadhi wanakuwa na uelewa.

Anafafanua kuwa, Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) Kanda ya Kusini, imekuwa ikijitahidi kutoa elimu ya uhifadhi, ingawa haiwafikii wananchi wote, kwa kuwa inatolewa katika ngazi ya kata.

Gaudai anaiomba taasisi husika kutoa elimu hiyo kwa ngazi ya kijiji, ili kuwawezesha wananchi kuipata pasipo kuwaogopa walinzi wa hifadhi na ana ufafanuzi:

"Kama wanavijiji vyote wakipata elimu kikamilifu, itachochea ushirikiano baina ya wanavijiji na hifadhi na kuondoa hofu. Hata inapotokea jambo limefanyika, wananchi inakuwa rahisi kuwajulisha watu wa hifadhi badala ya kuwaogopa," anasema.

Pia, anasema pale inapotokea suala la uhalifu katika hifadhi inakuwa ni rahisi kutoa ushirikiano kwa taasisi badala ya kuwaogopa.

### TEMBO WAHARIBIFU

Yassim Aloyce, mkazi wa kijiji cha Igava, anayesema wamekuwa wakivamiwa na wanyamapori na mazao yao kuliwa shambani na hadi sasa, wameshindwa kupata haki zao.

Analalamika kwamba, hawajui hatua za kufuata ili waweze kupatiwa kifuta machozi chao, ingawa wametoa taarifa za uharibifu katika ofisi za serikali za vijiji na mpaka sasa hawajapokea majibu yoyote.

Ofisa Mtendaji Kata ya Igava, Ibrahimu Mwakisopile, anasema amepokea malalamiko kuhusiana na wananchi kuharibiwa mazao yao na madai yao ameyawasilisha katika idara husika.

Kwa mujibu wa mtendaji huyo, ekari zaidi ya 50 ziliharibiwa na tembo katika kata hiyo na mpaka sasa hakuna mrejesho aliyoupata.

Mwakisopile anasema, wanyama wanapovamia katika maeneo ya wananchi, kumekuwapo ugumu utokanao na baadhi ya wanavijiji hawana elimu ya kukabiliana na wanyama hao.

Anasema, inapotokea wanavamiwa na tembo huwa wanatoa taarifa kwenye hifadhi au kuna wakati wanapiga ngoma, hivyo kelele zinamfanya tembo kuondoka.

"Tunahitaji mbinu zaidi katika kukabiliana na wanyama wengine ili wanapojitokeza kwenye makazi yetu tujue namna ya kuwaondoa wakiwa salama bila ya madhara," anasema Mwakisopile.

### KAMANDA HIFADHINI

Kamishna Msaidizi wa Hifadhi, kutoka Kanda ya Kusini, Pius Mzimbe, anafafanua kuna kitengo maalumu cha Ujirani Mwema ambacho moja ya majukumu yake ni kutoa elimu ya uhifadhi wa wanyamapori, ili kuimarisha uhusiano kati yao na wanavijiji wanaozunguka hifadhi.

Mzimbe anasema elimu imekuwa ikitolewa kwa vijiji, ingawa anakiri sehemu ya udhaifu wa baadhi ya wanavijiji hawatoi kipaumbele kunakohusika.

Anasema ofisi yake ina mikakati ya kuongeza nguvu kwenye elimu kwa wananchi ili kuimarisha ushirikiano uliokuwapo na anakiri uwapo wa tembo wavamizi katika maeneo ya wanavijiji, baadhi wakijenga nyumba kwenye njia za wanyama (Shoroba), hali inayochangia matatizo kama tembo kupita katika makazi yao.

Kamishna Msaidizi Mzimbe, anaeleza mazingira magumu ya wafugaji kuingiza mifugo hifadhini, ni hali inayohatarisha usalama kwa wanyamapori.

Anataja waalakini mwingine, ni uvuvi haramu katika hifadhi, akiwashauri kiwapo kasi ya kubuini mbadala wa kutengeneza mabwawa binafsi.

### MKUU WILAYA ANGA'KA

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, anasema kuna tatizo la baadhi ya wanavijiji wanatumia suala la elimu kama kisingizio cha kujitetea dhidi ya hujuma kwa mazingira ya hiofadhi, akisema halmashauri ya wilaya hiyo kwa kushirikana na TANAPA walipeleka wataalamu wa sekta husika na wananchi wanaozunguka hifadhi.

Mfune anasema, mikakati iliyopo ni kuongeza nguvu katika ya utoaji elimu kwa wanavijiji, ili washiriki kikamilifu kutunza hifadhi hiyo, akifafanua:

"Tunachokifanya kwa kiasi kikubwa ni kutoa elimu ya uhifadhi waelewe umuhimu wa hifadhi, lakini wajue mwingiliano kati ya wananchi na wanyama kwenda kwenye hifadhi. Kuna magonjwa ambayo mwingiliano ukitokea kuna madhara kwa hifadhi na mifugo inayoingizwa kwenye hifadhi."

"Kikubwa ni elimu! Mnyama hana mpaka, hifadhi ina mpaka... mnyama hana mpaka hawezi kusoma 'GPS' akajua hapa anakoenda ni makazi ya watu," anasema Mkuu wa Wilaya.

Anafafanua kwamba, kuna kambi za Ruaha zinazosaidia pale inapojitokeza magumu ya wanyama wanaoswagwa waweze kurudi katika hifadhi na kutosababisha madhara kwa wananchi.

Mfune anasema, waliopata madhara wanaendelea kuwashughulikiwa kupitia Kitengo cha Halmashauri ya Mbarali, waweze kufidiwa mazao yao yaliyoliwa.

"Kwa kiasi kikubwa mwingiliano huo pia umekuwa ukileta madhara kwa sababu wengi wanaamini ng'ombe wanapoingia katika bonde la ihefu, wanazaa kwa kiasi kikubwa. Hii imani imekuwa potofu, watu wameendelea kuwa nayo ndio maana wengi wanarudi na kupeleka mifugo," anasema Mfune.

Mfune anasema, mifugo mingi huwa inapelekwa majira ya usiku na inatolewa huko asubuhi jambo, ambalo katika upande wa pili haliruhusiwi kwa mujibu wa sheria.

"Yapo madhara mengine pamoja na elimu tunayoendelea kutokea, watu wanaamini zaidi katika kupambana yaani pale ambapo mifugo imekamatwa hawataki kufuata utaratibu,"anasema Mfune.

Anasema katika elimu wanayoitoa wanawaelimisha mifugo inapokuwa imekamatwa wafuate utaratibu unaotakiwa kufika kwenye kituo husika ama kulipa faini, ili aweze kuchukua mifugo yake.

Mfune anasema wananchi wanatakiwa kuzingatia mambo hayo ili kujiepusha kujiingiza katika migogoro katika hifadhi na atakayekamatwa atachukuliwa hatua.

Aidha, anasema hifadhi hiyo imetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika vijiji vinavyozunguka hifadhi za Kanda ya Kusini, ikiwamo ujenzi wa madarasa, bwalo la chakula kwenye shule ya Mawindi, bweni, kuwafungia mitambo ya umeme wa jua kwenye shule na kujenga visima vya maji.



Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune. **PICHA ZOTE: BEATRICE SHAYO.**



Kamishna Msaidizi wa Hifadhi Kanda ya Kusini, Pius Mzimbe (kulia), alipofafanua jambo.

MAZINGIRA

# Mabadiliko ya tabianchi yalivyo chanzo kubomoka madaraja Moro

## •Yamefikwa yaliyotarajia umri miaka 100
## •TANROADS: Shida kuu ni kilimo holela



Daraja la Mto Kilombero, mkoani Morogoro, katika mandhari mapya baada ya maboresho. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Christina Haule, Morogoro**

MABADILIKO ya tabianchi yana tabia ya kuchukua sura ya mageuzi mapya katika jamii na Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Morogoro (TANROADS) Mhandisi Nkolante Ntije, anasema lina jumla ya madaraja matano yamebomoka mkoani Morogoro katika kipindi cha mwaka 2018/2020.

Anataja sababu kuu ya kutokea hali hiyo, ni shughuli za kibinadamu zinazofanywa kwenye milima jirani na vyanzo vya maji, hapo ikitajwa kuongeza mashamba, hasa ya kilimo kisichokuwa rafiki.

Hapo inatolewa mifano, kwenye milima bila ya kuzingatia kilimo cha kinga za maji au kutochukua tahadhari zinazoweza kusababisha mmomonyoko wa ardhi.

Meneja huyo wa TANROADS Morogoro, Mhandisi Ntije anasema madaraja mengi yamekuwa yakibomoa kutokana na mvua kubwa zinazosukuma mchanga, magogo makubwa na kushuka kwenye mito na kuvunja kingo za madaraja, kufimia hatua ya kubomoka, hali inayohiyaji matengenezo makubwa.

Anasema, huwa wanakadiria uhalisia wa kile wanachokiangalia katika ujenzi kudumu kwa miaka 100 ijayo, pasipo mabadiiko ya kimazingira,

Mzee aliyesema hajawahi kuona hayo mafuriko na uharibifu uliojitokeza ambapo ana uhakika akifikisha miaka 90 ataweza kuona tena hayo ambayo huwa yanajirudia ambapo hali hiyo ya kujirudia ambayo kitaalamu huitwa (return period) huwa wanaitumia ili kuweza kukadiria ukubwa wa daraja linalohitajika mahali hapo.

**TANROADS MORO**

Meneja wa TANROADS, Mhandisi Nkolante Ntije anataja madaraja yaliyovunjika, ni pamoja na daraja la Itete lililopo Dumila, umbali wa kilomita 10 kutoka mji wa Kilosa, lililovunjika baada ya mvua kubwa kunyesha.

Anasema, ni athari ya kuvunjika kingo za daraja za zege na kufanya uharibifu mkubwa upande wa uelekeo wa maji ambayo yalichimba kina kirefu na kuliacha daraja linaling'inia.

Ntije anasema TANROADS ilichukua hatua za haraka, kupeleka wataalamu wake kurekebisha na ikabaki kazi ndogo kama za usafi.

Pia, anataja daraja lingine la Berega Wani lililopo kwenye barabara kuu iendayo jijini Dodoma kutoka Morogoro, lilidondoka Machi 2 mwaka huu na jitihada zilifanyika kutafuta mbadala wa kupita.

Anasema, hatua iliyofikia sasa, magari yameshaanza kupita hapo

> **Mhandisi huyo analitaja daraja la mwisho kuwa la Mwangaza, lililoko kwenye barabara ya Kiziwa-Tawa liliposombwa na maji, walitumia mbadala kuhakikisha watu wanaendelea na safari na ujenzi wake unaendelea.**

kwa kiwango cha lami na ujenzi wa daraja lenyewe unaendelea, chini ya usimamizi wa TANROADS mkoa, kwa matarajio utakamilika kabla ya mwaka huu kwisha.

Lingine ni kwamba, daraja la Kitope lililopo kwenye barabara ya Mvomero-Ndole- Kibati- Lusanga, lililosombwa na maji ya mvua zilizonyesha mwanzoni mwa mwaka huu, ambazo zilipitiliza kiwango kilichotarajiwa.

Mhandisi Ntije, anasema kwa sasa daraka hilo limekamilika na wanaendelea na utengenezaji njia za kuingia darajani, ili liweze kutumika.

Pia, anataja lingine kuwa ni daraja la Mjonga lililopo kwenye barabara ya Mvomero-Ndole- Kibati hadi Lusanga, lililobomoka wakati wa mvua na sasa limerudishwa daraja la chuma, kurejesha mawasiliano

Anasema, jitihada za kurudisha daraja jipya kubwa litakalokidhi maji hata ya mafuriko kupita, lipo kwenye hatua za ujenzi.

Mhandisi huyo analitaja daraja la mwisho kuwa la Mwangaza, lililoko kwenye barabara ya Kiziwa-Tawa liliposombwa na maji, walitumia mbadala kuhakikisha watu wanaendelea na safari na ujenzi wake unaendelea na ujenzi.

Anasema, kitaalamu suala la mabadiliko ya tabianchi, kuongeza mashamba hasa kwa kilimo kisichokuwa rafiki huongeza uharibifu wa mahali.

Pia, Ntije analitaja Daraja la Mkundi, limekamilika kujengwa mjini Morogoro, lakini kutokana na shughuli za kibinadamu kwenye mikoa ya Dodoma na Kondoa, mvua inapotokea husababisha mto badala ya kujaa maji, unajaa michanga na kuharibu daraja. Jitihada zinafanyika kuifanyia maboresho sahihi.

Aidha, anasema madaraja makubwa mara nyingi huwa na makadirio ya kudumu kwa wastani wa miaka 100 makadirio yanayojumuisha hata kiwango cha maji, kama hapatakuwapo madhara tofauti akitoa mfano wa Daraja la Kilombero.

Anasema wanapokadiria kiwango cha maji pia hukadiria miaka 100 itakayodumu, huku mkazi mmoja akitoa ushuhuda hajawahi kuona mafuriko na uharibifu uliojitokeza ambapo, katika umri wake wa miaka 90.

Meneja TANROADS anasema, muhimu ni kujengwa daraja la kudumu, kulingana na hali ya mto ulivyo na muhimu, ingawa kuna sura nyingine ya pili, kuhusu ugumu wa madaraja yanayobomoka kuwa na bajeti yake, maana ni ya dharura na si kinachotarajiwa

Hivyo, Injinia Ntije anatoa wito kwa maofisa kilimo kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Morogoro, kutoa maelekezo sahihi kwa wananchi kuhusu kilimo rafiki kwa mazingira.

Anasema, kukosekana elimu ya kilimo kinachohifadhi mazingira kwa wakulima, ndicho kinachotoa athari kubwa kwa namna moja au nyingine kwenye maeneo mbalimbali, ikiwamo kuharibu vyanzo vya maji na kubomoa madaraja.

**KATIBU TAWALA**

Katibu Tawala Msaidizi (Miundombinu), Mhandisi Hezron Charles anasema, Morogoro imo katika mikoa iliyobarikiwa mito mingi na una kiwango kikubwa cha mvua kinachonyesha, hali yenye athari ya madaraja mengi kuchukuliwa au kusombwa na maji na baadhi ya maeneo hayapitiki.

Anataja madaraja yaliyochukuliwa na maji kuwa ni daraja lililopo Wilaya ya Malinyi lililoharibiwa na kufanya kushindwa kupitika hata kwa gari, Daraja la Mlimba, lililopo barabara kuu ya kutoka Morogoro kwenda Dodoma; daraja la barabara kwenda hospitali maarufu ya Berega; daraja lililopo barabara ya kuelekea Mvuha wilayani Morogoro.

Anasema chanzo kikubwa kinachosababisha miundombinu ya barabara ikiwamo madaraja kushindwa kupitika ni wingi wa mvua na mito iliyopo mkoani hapo inayotiririsha maji na kusababisha madaraja kubomoka.

Mhandisi Charles anasema, sehemu kubwa ya madaraja yaliyopo ni ya zamani na yanahitaji matengenezo yapitike msimu wote wa mwaka, hivyo hapo ana kilio cha bajeti itengwe kufanikisha matengenezo makubwa na madogo yaliyopo sasa.

Pia, anasema serikali inaendelea kurekebisha madaraja, kadri inavyopata fedha za kazi hiyo, ikiwamo kupitia bajeti ya mwaka.

AFYA

# Dada 'chapombe' asimulia maisha ya ajabu... mengine yasiyoelezeka

- Aanza upya akiwapigia magoti wana
- Leo akiri nguvu ya wazazi imetenda



Caroline Kagia, katika picha tofauti. **PICHA: ZOTE MTANDAO.**

DADA Caroline Kagia, alikuwa ametimiza miaka 18, hivyo kisheria alikuwa mtu mzima. Lakini moyoni mwake, hakujiamini hata kidogo.

Dada huyo alidhani pombe ingemsaidia kumuongezea ujasiri, lakini badala yake alijikuta inamuogezea utumwa, shida iliyomfanya apambane kujikomboa kwa muongo mmoja na hata nusura apoteze maisha yake.

Caroline, haiba yake alikuwa mtoto mpole mwenye kuona haya mbele ya watu, akifafanua: "Upole ulinitia hofu, nilikuwa naogopa watu mno."

Baada ya kujiunga katika elimu ya sekondari, Caroline alipata rafiki mvuta sigara, pia alikuwa anakunywa pombe.

Yalikuwa mambo mageni kwa Caroline, kwani alilelewa katika misingi ya kidini, wazazi wake muda wote walisisitiza nidhamu kwake.

Caroline alijenga tabia ya uigizaji karibu na wazazi wake, lakini alijivunia uhuru wake faragha, akihamasishwa na rafiki yake aliyempatia chupa ya mvinyo.

Walibadilishana mawazo na mwishowe rafiki huyo alimfundisha pale wazazi wanalala, anywe 'kwa raha zake' chumbani kwake .

"Kileo changu cha kwanza kilikuwa chupa ya mvinyo (Redwine) yenye ujazo wa milimita 250. Hii ni pombe yenye nguvu ya asilimia 12," anakumbuka Caroline.

Kutokana na simulizi alizokuwa anasikia kutoka kwa marafiki zake, alihisi kinywaji hicho hakikutimiza matarajio yake, akieleza: "Sikulewa au kuonyesha dalili zozote za ulevi."

Anaeleza, mwili wake ulikuwa na uwezo kuhimili makali ya pombe na anakiri marafiki aliyokuwa nao wakati huo, waliwezesha kirahisi yeye kuhamia kwenye ulevi na akaufurahia.

Hata hivyo, nyumbani kwao hawakujua chochote kilichohusu ulevi wake na baada ya muda, Caroline alipata fursa kwenda masomo bara Asia.

Huko aliendeleza ulevi na baada ya mwaka mmoja, aliwapigia simu wazazi akidai mazingira ya nchi aliko ni magumu na ameshindwa kukamilishia masomo. Wazazi walimkubalia arudi.

Aliporudi kwao Kenya, wazazi hawakugundua, ila walibaini mwonekano wake ulibadilika sana. Hata hivyo, hisia za wazazi hazikuenda mbali, kwani kifunga mimba na kipenzi cha familia huyo, aliaminika sana kwa hoja zozoze alizotoa.

Baadaye, Caroline alijiunga na masomo ya uandishi wa habari katika chuo nchini kwao Kenya na akapata ajira iliyomuanzishia maisha rasmi.

**MAISHA TATA**

Caroline anasema, hali ilikuwa mbaya sana kwa siku ambazo hakutumia kilevi au kuvuta sigara, alihisi kana kwamba angepoteza ufahamu.

Anasema kuna wakati alishikwa na hali ya kifafa, inapotokea amelewa sana na siku inayofuata amekosa.

"Kwa kuwa nilikuwa nimeanza kunywa pombe kila siku, mara nyingi nilikuwa nikijifungia nyumbani kwangu. Nilichukia kushirikiana na watu kwa sababu nilihisi walikuwa wananihukumu," anasema na kuongeza:"Siku ambazo nilikunywa pombe, nilihisi mwenye furaha sana."

POMBE VS KAZI

Caroline, aliajiriwa katika taasisi moja alikotumikia kwa miaka 10, kati ya mwaka 2006 na 2016, ambaye kitaaluma alikuwa mbobezi katika aliyotumikia.

Siku zote alijizatiti kufanya kazi akiwa hodari kuliko wote. Lakini kila ulevi ulipoanza kumnyemelea, mara moja alihamia kwenye matokeo mabaya kazini.

"Sikuweza kutimiza malengo yangu katika mauzo kwa sababu sikuwa nikikutana na wateja. Nilikuwa kwenye baa kila wakati kutoka saa nne asubuhi.

"Lakini, ningewadanganya wakubwa wangu kupitia maandishi juu ya mikutano yangu ya siku hiyo na kujitokeza siku inayofuata kazini na hadithi za huku na kule," anakumbuka Caroline.

**VITUKO VYAKE**

Katika hali ya ulevi, mwanamke huyo anaelezwa kuwa na vitimbi na vituko vingi, mojawapo ni tabia ya kuwaacha watoto wake wamelala usiku na kuhamia kwenye vijiwe vya ulevi hadi usiku wa manane.

Pia, anadokeza kuna wakati alipoingia baadhi ya vilabu vya pombe pasipo kumjua hata mtu mmoja na hana pesa mfukoni, akitumai kulipiwa vinywaji vyake.

Anasimulia mikasa iliyomkuta kutokana na tabia yake ya ulevi kwamba:"Viatu vyangu vimechukuliwa kwa sababu sikuweza kulipia vinywaji vyangu. Niliwahi kufungiwa kwenye baa kwa siku nne kwa sababu sikuweza kulipia vinywaji vyangu.

"Siku ambayo mmiliki wa baa aliamua kunipeleka kituo cha polisi, nilipata njia ya kutoroka na sikuonekana tena katika eneo hilo."

Vituko vingine anavyovikumbuka ni pamoja na kumhadaa mhudumu wa baa kwa kumpa kifaa bandia cha kuchaji simu, akijifanya anaingia chooni na akatoweka bila kulipa.

Kwa mujibu wa Caroline, mkasa mwingine anaukumbuka ni alipouza vitu vyake vya nyumbani, kama vile milango ya nyumba, ili apate pesa za ulevi.

**ALIVYOBADILIKA**

Kukurukakara na vitimbi vya ulevi wake, vilimfikisha hatia atamani mabadiliko.

Vilevile, alipatwa na hofu ya hatima ya watoto wake wawili, pale wangeingia katika umri wa ufahamu na kujua yanayomhusu mama yao 'mlevi wa kupindukia.

Katika hilo, Caroline anakiri kuhisi kuwa mfungwa mwanamke, anayekosa mwongozo wa kuwapa watoto wake na hasa pale uhusiano wa kimapenzi ulipovunjika Novemba 2015, baada ya kukumbwa na ugomvi usioisha.

"Nilipunguza uzito haraka sana na nilivaa suruali mbili ili tu kuonekana kama nilikuwa na nyama kwenye mifupa yangu. Sikuweza kufikiria au hata kuongea, bila pombe katika mfumo wangu.

"Mnamo Januari 2017 mwishowe nilisema tosha na nikachukua uamuzi kwamba ilikuwa wakati wa kubadilika na kurudisha maisha yangu kuwa yenye mwelekeo," anasimulia.

**MABADILIKO**

Caroline anaeleza aliwaambia wazazi wake angetamani kupelekwa kwenye ushauri nasaha, mahali pa kuacha pombe na wazazi wake walimkubali wakampeleka kwenye kituo alikokaa miezi sita, alipotoka alishabadilika sana.

Kipindi alichokuwa mlevi, uhusiano wake na jamii ulizorota sana. Mtoto wake wa kiume alishuhudia vitimbi vingi kutoka kwa mama yake. Ilibidi amuite na kumuomba msamaha.

Ndani ya kipindi cha msamaha na mabadiliko kilikuwa na machozi mengi mno, kwa watoto na familia yake kwa jumla.

"Ninaamini nilivutiwa na pombe kwa sababu nimekuwa nikipambana na hali ya kutojithamini tangu utotoni. Mimi ni mzaliwa wa kwanza katika familia ya ndugu watano. Pamoja na haya yote, nilikuwa na hali ya kujiona mtu wa chini," anasimulia.

Wazazi wake walisimama naye katika safari ya kubadilika, akitaja mchango wa baba yake katika mabadiliko kuwa: "Katika safari yangu ya kupona baba yangu alikataa kabisa kuniacha.

"Aliendelea kuniangalia, kuniombea na kuzungumza mazuri juu ya maisha yangu. Baba yangu alibadilisha hatima yangu kupitia upendo wake usiyoyumba na usiokoma."

Anasema baba hakumlaani kamwe, isipokuwa kila mara alimbariki kwa maneno yake, huku akidokeza: "Nguvu ya ulimi ni ya kweli. Bila msaada mzuri, ni rahisi kurudi tena.

"Uraibu ni ugonjwa kama mwingine wowote, na unapaswa kutibiwa kama hivyo. Inawezekana kwa mraibu kupona kabisa lakini tu katika mazingira sahihi na kwa Msaada sahihi." BBC



# NARCO yaipa serikali gawio mil. 400/-

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMPUNI ya Rachi za Taifa (NARCO) imetoa gawio serikalini kwa kipindi cha miaka miwili ya 2018/2019 na 2019/2020 jumla ya Sh. milionio 400, kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni hiyo, Mipawa Mselle, alisema hayo wakati alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu mafanikio na mikakati ya NARCO.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano shirika hilo limefanikiwa kutoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kwenda katika mfuko mkuu wa serikali.

Pia, alisema kuwa toka kuanzishwa kwa kampuni hiyo, imepata mafanikio mengi ikiwa ni pamoja na kusambaza mbegu za mifugo kwa wananchi kwa kuwauzia kwa bei nafuu ukilinganisha na bei ya soko.

**NARCO, imefanikiwa kutoa mafunzo kwa vitendo ambapo imekuwa ikipokea vijana 1,000 kwa mwaka kwenye ranchi zote nchini.**

Kutokana na hali hiyo, wafugaji waendelea kupata madume na mitamba bora kwa urahisi na bei nafuu.

Vile vile, alisema NARCO, imefanikiwa kutoa mafunzo kwa vitendo ambapo imekuwa ikipokea vijana 1,000 kwa mwaka kwenye ranchi zote nchini.

Alisema, vijana hao wanatokea katika vyuo vya elimu ya juu na kati, vyuo vya mifugo, sekondari na shule za msingi kwa ajili ya mafunzo ya vitendo na utafiti katika fani mbalimbali za sayansi ya mifugo na kilimo, mazingira, biashara, uwekezaji na ufugaji kisasa na kibiashara.

Mafanikio mengine, alisema ni kutoa ushauri wa kitalaamu bure kwa wananchi unaojumuisha kinga na tiba za magonjwa ya mifugo, unenepeshaji wa mifugo na malisho bora ya mifugo.

Pia uzalishaji na uendeshaji wa shamba la malisho na ranchi ndogondogo, uhamilishaji na uandaaji wa utunzaji wa nyama bora.

"NARCO pia imefanikiwa kuzalisha na kuuza kwa wananchi malisho bora na ya uhakika kwa bei nafuu hasa kwa ajili ya wananchi wenye mifugo inayofugwa mijini na wakati wa kiangazi, ambapo kunakuwa na uhaba mkubwa wa malisho," alisema Masele.

Aidha, alisema kwa upande mwingine katika jitihada za kuimarisha mahusiano mazuri kati ya kampuni na jamii za wafugaji wanaozunguka maeneo ya ranchi, wamewapangisha kwa mikataba mifupi na hii imesaidia wafugaji kutohamahama na mifugo kutafuta malisho na maji.

Pia, alisema hali hiyo imesaidia kiasi cha ng'ombe 31,356, mbuzi 11,733 na kondoo 6,000 kutoka katika vijiji 30, kote nchini wamepata huduma katika ranchi za NARCO.

Kadhalika, alisema kuwa wamefanikiwa kuzalisha na kutunza mbegu bora ya ng'ombe aina ya boran ambao wanakua haraka ukilinganisha na aina zingine za asili ambao huvunywa mapema zaidi.

"Serikali imeendelea kujivunia zao la boran na kuhimiza uzalishaji wa madume kwa ajili kuwauzia wafugaji ili waboreshe mifugo yao ya asili tangu kampuni ianze miaka ya 1968 na imekuwa ikizalisha ng'ombe wa nyama aina ya boran," alifafanua.

Alisema wamefanikiwa kutoa huduma ya maji kwa wananchi na mifugo hasa wakati wa kiangazi katika mikoa tisa mahali zilipo ranchi, ambapo zaidi ya wananchi 2,500 na mifugo zaidi ya 30,000 hunufaika na maji yanayopatikana katika visima na vyanzo vingine bure.

## Askofu afunda waliogombea uchaguzi mkuu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU mstaafu wa Kanisa (EAGT) la Ipagala, Dk. Evance Chande, amewataka wagombea wote kuanzia nafasi ya udiwani hadi urais, kukubali matokeo na wasidanganyike na wingi wa watu wakati wa mikutano ya kampeni.

Rai hiyo, ilitolewa na Askofu huyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uchaguzi mkuu uliofanyika nchini mwezi uliopita.

"Wingi wa watu usiwadanganye wagombea kuwa wameshinda na kuanza kuaminisha umma, hawa ndio wajumbe bwana ambao wanaweza kufanya chochote kile wanachoona kinafaa, tukumbuke kuwa kuna maisha baada ya uchaguzi," alifafanua Askofu Chande.

Pia, askofu huyo aliwapongeza Watanzania kwa kutojihusisha na maandamano kuingia barabarani kufanya vurugu kama ambavyo baadhi ya viongozi wa siasa walivyokuwa wakishawishi.

"Niwapongeze Watanzania kwa kutoshiriki maandamano yoyote hivi sasa hadi leo, ambapo Rais mteule ataapishwa, haki za binadamu bila kufuata sheria ni wendawazimu," alidai Askofu Chande.

Aidha, aliipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kwa namna ilivyoboresha zoezi la upigaji kura mwaka huu wa uchaguzi mkuu.

"Kitendo cha kuruhusu watu watumie vitambulisho vya taifa, leseni za udereva na pasi za kusafiria kumesaidai kutoa fursa ya watu wengi kushiriki katika kupiga kura," alisema.

Mkazi wa Swaswa jijini Dodoma, Livingstone Mmari, aliipongeza NEC kwa namna ilivyo wawajibisha wagombea ambao walikuwa wakitumia lugha za uchochezi katika mikutano yao ya kampeni.

Hata hivyo, alisema kuwa huu ni uchaguzi wake mkuu wa tisa kushiriki, lakini hakuwahi kuona mikutano ya kampeni yenye lugha kali kama mikutano ya kampeni za mwaka huu.

Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya Baraza la Waislamu (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma Mjini, Bashiru Husseni, aliwataka wabunge waliochaguliwa katika bunge lijalo kufanya kazi ya kuwawakilisha wananchi.



Mjasiriamali wa bidhaa za vyakula akimhudumia mteja wake huku akiwa amezipanga chini kwenye vumbi katika eneo la Uhindini, jijini Dodoma jana, kitendo kinachoweza kuhatarisha afya ya mlaji. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Vijana wa mazingira wampongeza JPM

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

VIJANA wa kikundi cha kutunza na kuhifadhi Mazingira cha Chapakazi jijini Dodoma, kimempongeza Rais mteule wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli (pichani), kuchaguliwa kuwa Rais, kwa awamu ya pili.

Aidha, kikundi hicho kimeahidi kuendelea kumpa ushirikiano Rais Magufuli katika kuchapa kazi na kusukuma gurudumu la maendeleo.

Kikundi hicho ambacho kinajishughulisha na upandaji wa miti, upandaji wa bustani ambacho kimetoa ajira kwa vijana zaidi ya 50, wa jijini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, mwenyekiti wa kikundi hicho, Khalid Hamadi, alisema wanampongeza Rais Magufuli kwa kuchaguliwa katika muhula wa pili.

Mwenyekiti huyo alisema wakiwa kama vijana waliojipambanua kwa kufanya kazi ya kuzalisha miche ya miti wataendelea kufanya kazi kwa bidii ili kushiriki katika mchango wa kuleta maendeleo nchi.



Alisema kijana anayelalamika kwamba maisha ni magumu ni yule ambaye hafanyi kazi na kuendelea kukaa vijiweni bila shughuli rasmi ya kufanya.

"Tunampongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais, tunajivunia kazi zake sisi vijana tunaojishughulisha maisha yetu yamebadilika, tunazidi kumwombea kwa mungu azidi kumpa maisha marefu," alisema.

Alisema kuwa, imani yao ni kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo ya Rais, Magufuli hali itazidi kuwa nzuri zaidi na ilivyokuwa katika muhula wa kwanza wa utawala wake.

"Bado tuna changamoto ya watu kutokuwa na uelewa kuhusiana na upandaji miti na kutunza mazingira, lakini sisi tumekuwa tukifanya kwa vitendo," alisema.

Aidha, walimpongeza Mbunge Mteule wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, kwa kuchaguliwa kuliongoza Jimbo la Dodoma Mjini kwa miaka mingine mitano.

Mwenyekiti huyo, alisema wana imani naye kutokana na kuwaongoza vyema kwa kuwasaidia vijana wengi kupata ajira pamoja na mikopo ya riba nafuu kutoka taasisi mbalimbali za kifedha.





# Bei ya dhahabu yapaa soko la Chunya

Na Grace Mwakalinga, CHUNYA

BEI ya dhahabu katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya imepanda hadi kufikia kiasi cha shilingi 142,000 kutoka shilingi 50,000 kwa gramu moja, hivyo kuvunja rekodi ambayo haijawahi kutokea tangu kuanzishwa kwa soko hilo.

Bei hiyo imepaa ikiwa ni siku chache baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu, na kuvunja rekodi ambayo haijawahi kufikiwa tangu kufunguliwa kwa soko hilo ambalo linatumiwa zaidi na wachimbaji wadogo kuuza madini yao.

**Awali tulikuwa tunauza dhahabu kwa shilingi 50,000, lakini sasa kuna zaidi ya shilingi 100,000 hatupati tena shida...**

Hayo yalithibitishwa na Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Wadogo wa Madini wilayani Chunya, Leonard Manyesha, alipotembelea soko la madini ambapo alisema uwapo wa amani na utulivu nchini baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu, kumesababisha bei ya dhahabu kupanda, hivyo akawataka wachimbaji wadogo kudumisha amani na kufanya kazi kwa bidii ili wanufaike na ongezeko hilo la bei.

"Awali tulikuwa tunauza dhahabu kwa shilingi 50,000, lakini sasa kuna zaidi ya shilingi 100,000 hatupati tena shida tunaishukuru serikali kwa kuandaa utaratibu mzuri kwani ni rafiki kwetu...bei ambayo ni sawa na soko la dunia," alisema Manyesha.

Baadhi ya vijana hususani waendesha bodaboda na bajaji wilayani Chunya nao walisema kuwa na wao wananufaika na ongezeko hilo la bei ya dhahabu, kutokana na kuwahudumia wateja wao ambao ni wachimbaji wadogo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Mayeka, alisema wilaya hiyo inazo fursa nyingi za kiuchumi, hivyo aliwataka wananchi kuachana na siasa na badala yake watumie fursa hizo kwa kufanya kazi ili wanufaike.

Aliwaomba wachimbaji hao kuendelea na shughuli zao za kutafuta dhahabu kwa bidii badala ya kushawishiwa na wanasiasa kufanya maandamano ambayo yatawapotezea muda.



Mkazi wa eneo la Mwansekwa, jijini Mbeya, akiwa amesheheni majani ya kulisha mifugo kwenye baiskeli yake, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Chalamila ataka kasi uzalishaji wa saruji

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewaomba wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda vya kutengeneza saruji kuongeza kasi ya uzalishaji wa bidhaa hiyo ili kukidhi mahitaji ya watumiaji.

Pia amewataka kupunguza bei ya uuzaji kutoka Sh. 22,000 hadi 25,000 kwa mfuko mmoja badala ya Sh. 18,000 ya awali.

Chalamila alitoa ombi hilo juzi wakati wa kikao na viongozi mbalimbali wa dini, wafanyabiashara na taasisi mbalimbali za mkoa huo, ambapo alisema kwa kipindi cha wiki tatu sasa bei ya saruji imepaa sana ukilinganisha na ilivyokuwa awali.

Alisema wazalishaji wengi wa bidhaa hiyo hususani kwa Kiwanda cha Mbeya Cement, waliamua kusitisha shughuli za uzalishaji kwa kipindi cha wiki tatu sasa, ili kupisha shughuli za uzalishaji hali iliyosababisha bidhaa hiyo kupanda mitaani.



Alisema kutokana na hali hiyo, wafanyabiashara nao walitumia mwanya huo kuuza kwa gharama kubwa ili kupata faida zaidi bila kujali hali za Watanzania.

"Nawaomba wamiliki wote wa viwanda vya saruji na wafanyabiashara Mkoa wa Mbeya turudi kuzalisha bidhaa hii kwa wingi kwani mahitaji ni makubwa huko mtaani watu wanauziwa kwa bei kubwa kwa sababu wengine wanafurahia hali hii ili waendelee kupiga hela," alisema Chalamila.

Mdau wa maendeleo wilayani Chunya, Lawena Nsonda, aliwaomba wafanyabiashara kuacha tabia ya kufungia bidhaa ndani wakisubiria bei kupanda.

Alisema kipindi cha uchaguzi wafanyabiashara wengi walifungia bidhaa zao wakihofia hali ya uchaguzi licha ya kupongeza kuwa ulifanyika kwa amani na utulivu hivyo sasa wanapaswa kufungua biashara zao kuendelea na maisha kama ilivyokuwa awali.

Aliongeza kuwa kwa sasa bidhaa nyingi zimeadimika na nyingine huuzwa kwa bei ghali ukilinganisha na hali za Watanzania hushindwa kumudu, hivyo aliiomba serikali kuingilia kati suala hilo.

## Wajasiriamali watakiwa maadili

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

WAJASIRIAMALI katika mikoa ya Mbeya na Songwe, wametakiwa kufuata maadili ya biashara ili kuhakikisha soko la bidhaa kutoka ndani na nje ya nchi linakuwa la ushindani pamoja na kukidhi matarajio ya walaji.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alipokuwa akizungumza na watu wenye ulemavu wa kusikia kutoka mikoa ya Mbeya na Songwe kwa lengo la kuwapatia elimu ya utambuzi wa bidhaa bandia.

Ntinika alisema kundi hilo la watu wenye ulemavu linapaswa kupewa elimu sahihi ya utambuzi wa bidhaa feki ili kuwasaidia kuepukana na madhara ya kiafya, lakini hasara katika biashara zao wanazozifanya.

Alisema elimu ya utambuzi kwa kundi hilo ni endelevu ili kuwafikia na wengine waishio pembezoni ambao kutokana na jiografia, hali zao na na ukata wa fedha ni vigumu kupata elimu hiyo licha ya kuwa baadhi yao ni wafanyabiashara na wateja wa bidhaa mbalimbali.

"Bado kuna haja ya kuendelea kutoa elimu ya utambuzi wa bidhaa bandia kwa kundi la watu wenye ulemavu kwa sababu kutokana na hali walizonazo ni rahisi kupata madhara ya kiafya au kupata hasara ya kibiashara kinachohitajika sasa ni kuunganisha nguvu za pamoja kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kufikia vijijini kutoa elimu hiyo," alisema Ntinika.

Baadhi ya watu wenye ulemavu wa kusikia walisema ukosefu wa elimu ya utambuzi wa bidhaa bandia sokoni una athari kubwa kwa kundi hilo ikiwemo kuhatarisha uhai, lakini pia kupata hasara pindi bidhaa zao zinapokamatwa na mamlaka zinazohusika.

Mwanyekiti wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) Mkoa wa Mbeya, Tusekile Mwalwega, alisema yeye ni miongoni mwa waathirika wa matumizi wa vipodozi feki ambavyo viliingizwa kinyemela nchini.

Alisema alipata madhara ya ngozi yake baada ya kupakaa mafuta ambayo yalipigwa mafuruku na kwamba hakuwa na taarifa zozote juu ya marufuku hiyo.

Kutokana na mazingira hayo, alisema athari inaweza kuwa kubwa kwa wenzake ambao hawana uwezo wa kusoma na kuandika lakini upatikanaji wa habari kwao ni tatizo hivyo njia pekee ya kuwasaidia kuwafikia waliko na kuwapa elimu.

Hivi karibuni Mkurugenzi wa Udhibiti Bidhaa Bandia kutoka Tume ya Ushindani nchini, Godfrey Mshana, alisema kundi la viziwi lina mahitaji maalum hivyo linahitaji ulinzi dhidi ya athari za bidhaa bandia sokoni.



## Kongamano la amani laandaliwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISI ya Mufti Zanzibar imesema inatarajia kufanya kongamano la kuhimiza amani, upendo na mshikamano baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa Oktoba, 28 mwaka huu.

Katibu wa Mufti, Sheikh Khalid Ali Mfaume, alisema jana kuwa lengo la kongamano hilo ni kuwaunganisha wananchi na kuwataka kuacha chuki, ubinafsi baina ya wafuasi wa vyama vya siasa.

Alisema wako wananchi walioanza kuwekeana visasi baada ya kumalizika kwa uchaguzi na kutangazwa mshindi, hivyo kongamano hilo litawaunganisha pamoja na kutokuwa na mifarakano kati yao.

Sheikh Khalid alisema watendaji tayari wameanza kuratibu mipango ya kongamano hilo na itakapokamilika ofisi itatoa taarifa rasmi kwa wananchi kuwataka kushiriki.

Kauli ya katibu huyo imekuja kutokana na kuwapo kwa taarifa za baadhi ya wananchi kuwekeana visasi ikiwamo kutoshiriki mazishi kwa sababu za kisiasa.

Hata hivyo, alisema wataendelea kutoa maelekezo yenye kuhimiza amani kupitia vikao vya dini na nyumba za ibada licha ya harakati za uchaguzi kumalizika.

"Tunaposhuhudia matukio kama haya, ofisi yetu inalazimika kuchukua jitihada za kuwaunganisha wananchi na kuwa kitu kimoja," alisema.

Aliwataka wananchi kuendelea kushikamana kwa kufanya mambo ya kijamii na uchaguzi umekwisha na kilichobakia kuendelea na tamaduni zao walizojiwekea.

Katibu huyo pia alikemea tabia ya kuhusudiana baada ya kuteuliwa kwa viongozi walioingia madarakani wakiwamo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wabunge, wawakilishi na madiwani.

## Dk. Mwinyi ateua Mwanasheria Mkuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameanza kujaza safu za uongozi katika serikali yake kwa kumteua Dk. Mwinyi Talib Haji kuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.

Dk. Mwinyi alifanya uteuzi huo juzi kwa mujibu wa kifungu namba 55 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ikiwa ni siku moja toka aapishwe kushika wadhifa wa Rais Novemba 2, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Dk. Abdulhamid Yahya Mzee, kabla ya uteuzi huo Dk. Haji alikuwa Naibu Katibu Mkuu katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Uteuzi huo umeanza Novemba 3, mwaka huu, na kwamba kabla ya kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Julai, mwaka huu, Dk. Haji alikuwa Mkuu wa Chuo cha Utawala wa Umma (IPA).

# Elimu udhalilishaji yawaibua wanafunzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa mtandao wa kupinga udhalilishaji wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Fatma Khamis Ali, amesema wanafunzi wamekuwa na uelewa mpaka kuhusu udhalilishaji baada ya kupata elimu.

Akizungumza jana katika Shule ya Msingi Mfenesini, Fatma alisema awali wanafunzi walikuwa hawana elimu kuhusu udhalilishaji, hivyo elimu waliyowapatia imeibua kesi nyingi ambazo wamezieleza.

Baadhi ya wanafunzi hasa wa shule za msingi, alisema waliwahi kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji, lakini kesi hizo hazijaripotiwa kutokana na wazazi kuzificha kutokana na sababu mbalimbali.

> **Tukitaka kutoa elimu huwa tunatakiwa tupeleke barua katika Baraza la Manispaa husika. Sasa barua hizo huchelewa kujibiwa na wakati mwengine kutojibiwa kabisa.**

Alizitaja miongoni mwa sababu za wazazi hao kushindwa kuziripoti kesi za udhalilishaji katika vyombo vya sheria ni muhali kwa sababu wafanyaji wa vitendo hivyo ni watu wa karibu katika familia.

"Zipo kesi mbili ambazo tumeziibua katika Shehia ya Nyamazi. Watoto wamefanyiwa vitendo vya udhalilishaji lakini wazazi wao hawakuziripoti katika vyombo husika na badala yake walizitatua wenyewe katika ngazi za familia," alisema Fatma.

Alisema baada ya wanafunzi kupata elimu hiyo, wamekuwa na uelewa wa kuzijua kesi ambazo zilikuwa hazijaripotiwa katika vituo vya polisi.

Katika utoaji wa elimu hiyo, alisema kumekuwa na changamoto zinazowakabili ikiwamo urasimu kwa baadhi ya shule kwa sababu wanapopeleka ombi lao la kutoa elimu huchelewa kujibiwa.

"Tukitaka kutoa elimu huwa tunatakiwa tupeleke barua katika Baraza la Manispaa husika. Sasa barua hizo huchelewa kujibiwa na wakati mwengine kutojibiwa kabisa," alisema.

Sida Omar Kombo, Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Mfenesini, aliwataka watoa elimu ya udhalilishaji kufika mara kwa mara shuleni hapo kutoa elimu hiyo kwa wanafunzi kwa kuwa elimu hiyo ni muhimu sana kwao.

Aliwataka wazazi na walezi kutoa ushirikiano kuwafichua wadhalilishaji ili kuchukuliwa hatua za kisheria zinazostahiki na watoto kuepuka kufanyiwa udhalilishaji.




Baadhi ya watalii wakiandika taarifa zao katika nyaraka za uhamiaji wakati walipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, Kisauni Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Dk. Shein: Uchaguzi 2020 umevunja rekodi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 yamevunja rekodi ya uchaguzi uliofanyika nchini kabla na baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964.

Dk. Shein alisema hayo juzi wakati wa kikao cha Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM Zanzibar kilichofanyika katika Ofisi Kuu ya CCM, Kisiwandui.

Alisema tangu enzi za siasa za ukoloni, Afro Shiraz (ASP) na baadaye CCM, chama hakijawahi kupata ushindi mkubwa kama huo jambo ambalo linapaswa kupongezwa na kila mpenda demokrasia.

Dk. Shein ambaye ni Rais mstaafu wa Zanzibar, alisema hatua hiyo imechangiwa na wagombea wote wa CCM kuwa imara na chama hicho kuwa na ilani na sera zinazouzika kwa wananchi. Alisema hali hiyo imetoa nafasi kwa wananchi kufanya uamuzi sahihi.

Aidha, aliwasihi wajumbe wa kikao hicho kutobweteka na ushindi uliopatikana badala yake waanze mapema maandalizi ya uchaguzi ujao utakaofanyika baada ya miaka mitano.

"Kwa ujumla ninawashukuru wana CCM na wananchi kwa ujumla kwa kufanya uamuzi sahihi wa kuichagua CCM ili iwaletee maendeleo endelevu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii," alisema.

Aliwaambia wajumbe hao kuwa amefarijika kuona amefika ukomo wa utumishi katika urais kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na kukabidhi madaraka hayo kwa Dk. Hussein Ali Mwinyi nchi ikiwa salama.

Dk. Shein alisema hana shaka na mrithi wake na kuamini kuwa atawatumikia Wazanzibari na Watanzania kwa haki, nidhamu na bidii huku akilinda tunu za taifa ukiwamo Muungano na Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Kikao hicho kilichokuwa na agenda moja ya kujadili na kutoa mapendekezo ya wanachama wa CCM walioomba nafasi ya Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Aidha, kikao hicho kilipokea na kujadili majina ya wanachama watano wa CCM waliojitokeza kuomba kuteuliwa kugombea nafasi hiyo inayoshikiliwa na Zubeir Ali Maulid.

Mbali na Maulid, wanachama wengine waliojitokeza kuomba nafasi hiyo ni aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa Baraza hilo, Mahamoud Mohammed Mussa, Yussuf Suleiman Khalfan, Tum Abdi Ali na Dk. Ameir Haidar Mshenga.

Majina yao yalijadiliwa na baadaye kupendekezwa katika vikao vingine vya juu vya chama kwa uteuzi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA NA MASHAMBA

**MATHEMATICS TUITION.** Mlete kijana wako tufuatilie msingi wake wa hisabati hadi pale shida ilipoanzia na kuanza kuujenga tena upya. Wahusika ni kuanzia darasa la tano hadi kidato cha sita.Tuitions za majumbani zinapatikana pia. Tupo Bunju Mwisho Dsm. Simu 0655.0754 617987 na 0782 461858

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTELEWA NA VYETI



**ABEL DAUD MILALI**
Amepotelewa na vyeti vya **kidato cha nne,result slip,leaving certificate,admission letter** na **cheti cha kidato cha nne** vyenye index namba **S1525/0026** vilivyotolewa na shule ya sekondari **KASANGE** mwaka **2019** yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DAR/MAG/RB/778377/2020**

## KUPOTELEWA KWA CHETI



**BRIAN DENNIS MREMA** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye namba **TZ016/0029** kilichotolewa na **DAR ES SALAAM INDEPENDENT SCHOOL (D.I.S)** mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Control No:
**9910819568412.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;331/2020**

**Ombi la EMERENSIANA B MAKATA, Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu BALTAZARY CHRISTOPHER MAKATA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/12/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/11/2020.

115975702

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NEELAM ABBASALI DATOO**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI **T742 DDQ**
CHASSES NO ANH **1001082020**
ENGINE NO **2A21819821**
YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI
**ARU/ARU/RB/772275/2020**

## NOTICE OF DATE OF MENTION:

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA AT BUKOBA**

**MISC. LAND CASE APPLICATION No. 98 OF 2019**
**(From the decision of the DLHT Bukoba Land Case No. 189/2018)**

WINIFRIDA FELICIAN ..........................................APPLICANT
**Versus**
**SEPERATUS KAST** ..........................................RESPONDENT
**GEORGE KAMANZI** ..........................................RESPONDENT

**TO GEORGE KAMANZI**
**NOTICE OF DATE OF MENTION:**

**TAKE A NOTE** that the above case has been fixed for Mention on the **28th Day of December 2020** at **9:00** am before **Hon. N.N. Kilekamajenga Judge.**
YOU ARE required to appear in this court on the fixed date without fail.
Given under my hand and the seal of the court this **26th Day of October 2020.**

**DEPUTY REGISTRAR**
**BUKOBA**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LETICIA KIJA MAKUNE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.5375-0009** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KUSEKWA MEMORIAL SEKONDARI** mwaka, 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **SIM/BAR/RB/574629/2020.**

115976802

## KUPOTEA KWA CHETI



**VERONICA KISHA,** anatangaza kupotelewa na vyeti,cheti cha kidato cha nne **index No S.2453/0047** kilichotolewa na shule ya sekondari MPUI mwaka 2016,cheti cha kidato cha nne chenye index No.**P.0660/0209.** kilichotolewa na **MOROGORO TEACHERS COLLEGE** mwaka 2017. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote na polisi. Taarifa ya polisi:**DOD/DOD/RB/416817/2020.**

115976502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JONATHAN IRIRA**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA** yenye namba za usajili **T 614 CKM** chasis namba **ACN100006346** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa control No
**9910819572151**

115976602

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA (W) MTWARA**
**MKOA WA MTWARA**

**MAOMBI NA. 79/2019**

**MAJID AHMED NASSOR..........................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**STANSLAUS KISAKA....................MJIBU MAOMBI NA. 1**
**SALOME PAUL NOBERT .............MJIBU MAOMBI NA. 2**

**KUITWA SHAURINI**

SALOME PAUL NOBERT, POPOTE ULIPO, FAHAMU kwamba shauri hili limepangwa kusikilizwa tarehe 17 Novemba, 2020 saa 02:00 asubuhi. UNAAMRIWA kuhudhuria mbele ya Baraza lililopo katika jengo la Baraza Idara ya Ardhi Manispaa ya Mtwara siku hiyo bila kukosa, wewe au mwakilishi wako kisheria. Hati ya madai pamoja na vielelezo vingine vyote kuhusiana na shauri hili utavipata kwenye masjala ya Baraza. FAHAMU KWAMBA kushindwa kuhudhuria Barazani siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja na kuamriwa dhidi yako. Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza leo tarehe 02 Novemba, 2020.

H. ILLUKEHA
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MTWARA.

115975202

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**AMOS JOHN SIMCHIMBA**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI CANTER** rangi nyeupe yenye namba za usajili **T 253 BAU.** Chassis namba **FE517BD522810** Engine namba **4D33F03844.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.Taarifa ya polisi
**MBE/MBE/RB/777063/2020**

115975602

## KUPOTELEWA NA CHETI



**ERICK SIAJALI,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2425/0092** kilichotolewa na baraza la taifa la mitihani kupitia shule ya secondary ya SUNRISE mwaka 2017, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **MWA/NY/RB/739750/2020**

115975502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo KINGOLWIRA.**

**Usimamizi wa mirathi No;25/2020**

**Ombi la IRMINA JAKA MICHAEL,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MICHAEL WILLIAM JAKA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

115976002

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT DAR ES SALAAM**
**MISC. CIVIL APPLICATION NO. 305 OF 2020**
**(Original from District Court of Kinondoni at Kinondoni in Civil Case No. 33 of 1999)**
**SALIM OMARI SALIM AND ZUBERI MBWENI**
**(Administrators of the estate of the late**
**MARIAM SELEMANI)**...........................APPLICATIONS
VERSUS
**ALLY MOHAMED HANIU** (Administrator of the estate of the late
**HIDAYA JUMA HANIU)**................**RESPONDENT**
**TO: ALLY MOHAMED HANIU – DAR ES SALAAM.**
**SUMMONS FOR PUBLICATION**

**WHEREAS**, the above mentioned applicant/plaintiff has instituted an Application against you at the High Court of Tanzania **(Dar es salaam Registry)** the facts of which may be found on request in the court file; You are hereby summoned to appear in this court in person or by a pleader duly instructed and able to answer all material questions relation to the Application or who shall be accompanied by some person able to answer all questions on 19th day of November, 2020 before **Hon. L. M. MLACHA, JUDGE** to answer the claim. You must be prepared to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your defense. **TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that day aforementioned, the Application will be heard and determined in your absence.
**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of court this **19th day of October, 2020.**




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Uhuru Kenyatta sasa azuia mikutano ya siasa

**NAIROBI,** Kenya

KENYA imepiga marufuku mikutano yote ya kisiasa kwa siku 60, ili kuzuia kuenea kwa virusi vya corona.

Akizungumza baada ya mkutano wa kuangazia hali ilivyo nchini humo, Rais Uhuru Kenyatta alisema jana kwamba ni kama viongozi wameshindwa kuwaongoza raia kufuata na kuheshimu masharti ya kukabiliana na corona yaliowekwa.

"Tumefeli kama viongozi kuhakikisha kuwa kuna kutokaribiana na kwamba watu wanavaa barakoa na kuosha mikono mara kwa mara."

Rais Kenyatta alisema kwamba viongozi wa kisiasa wanaweza kuandaa mikutano yao katika kumbi mbalimbali kwa kuhakikisha kwamba wanafuata maagizo ya kukabiliana na ugonjwa huo.

Alisema mikutano hiyo inapaswa kuwa na theluthi moja ya idadi ya watu inayofaa kujaza kumbi hizo. **BBC**

## Jeshi laagizwa kujibu shambulizi

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, aamuru jeshi kuendesha operesheni ya kujibu shambulizi dhidi ya kambi ya vikosi vya jeshi lililofanywa na vuguvuvu la chama tawala kwenye eneo tete la mkoa wa Tigray.

Katika ukurasa wake wa Twitter na Facebook jana, Abiy aliandika kuwa chama hicho TPLF kimeshambulia kambi ya jeshi kwenye mkoa huo na kujaribu kupora vifaa vya kijeshi.

Abiy ameonya kuwa kile kilichotokea kinapaswa kujibiwa vikali na tayari amelitaka jeshi kuchukua hatua nzito za kulinda taifa hilo.

Alisema shambulizi la TPLF ni kipimo cha mwisho cha uvumilivu wa serikali.

Haijafahamika mara moja hatua zipi za kijeshi zitachukuliwa, lakini wachambuzi na wana diplomasia wameonya kuwa makabiliano kati ya serikali kuu na chama cha TPLF yanaweza kuanzisha machafuko.

Chama cha TPLF kimehodhi siasa za Ethiopia kwa miongo kadhaa kabla ya Abiy kuchukua madarakani mwaka 2018 baada ya maandamano makubwa ya kuipinga serikali. **DW**

## Iran yataka eneo lake kurudishwa

**TERHAN,** Iran

KIONGOZI wa juu wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei (pichani chini), amesema kwamba eneo linaloshikiliwa na Armenia ndani ya Azerbaijan linapaswa kurejeshwa na kuonya kwamba mgogoro jimboni Nagorno-Karabakh unatishia usalama wa kikanda.

Khamenei aliyasema hayo jana katika hotuba kupitia televisheni, na kuongeza kuwa hilo ni sharti muhimu. "Bila shaka ardhi za Azerbaijan zilizochukuliwa na Armenia zinapaswa kukombolewa kikamilifu na kurejeshwa kwa Azerbaijan.

Hili ni sharti muhimu. Ardhi hizi ni za Azerbaijna na ina haki ya kuzikomboa. Zinapaswa kukombolewa. Na usalama wa Waarmenia wanaoishi kwenye ardhi hizi unapaswa kulindwa. Pia, mipaka ya kimataifa inapaswa kuheshimiwa."

Iran inapakana na Armenia na Azerbaijan na Tehran imeweka majeshi kwenye mipaka yake kutokana na athari za mapigano ndani ya mipaka yake.

Iran ina mahusiano mazuri na mataifa yote mawili na imeyatolea wito mara kwa mara kusitisha uhasama na imejitolea kusimamia mazungumzo kati yao. **DW**

AGRIBUSINESS INNOVATION CENTER AIC TANZANIA

PASS PRIVATE AGRICULTURAL SECTOR SUPPORT

# REQUEST FOR QUOTATION

## PROPOSED CONSTRUCTION OF OFFICE BUILDING FOR PASS AIC SUA - MOROGORO

**Date: 21st October 2020**

**Request for quotation**

1. The PASS TRUST has allocated a budget to cover various payments for Supervision and Construction of office building for PASS AIC SUA – MOROGORO. The aim of the project is to construct own office building premises for PASS AIC SUA - Morogoro.

2. The PASS TRUST now invites quotation from eligible "individual l**ocal fundis" and/or building contractors registered with the contractor's Registration Board** in Tanzania for carrying out the works for Proposed Construction of Office building for PASS AIC SUA – MOROGORO.

3. Tender documents are found in four different lots as described hereunder: -
   **a)** Lot I: Office Building
   **b)** Lot II: Toilets building
   **c)** Lot III: Guard house, security hut and Fence
   **d)** Lot IV: Civil works and external services

4. Interested bidders are allowed to quote/price for more than one Lot and the same to be submitted using the e-mail/link provided in 7 below.

5. A complete set of request for quotation Documents in English language and additional sets may be obtained by bidders though https://pass.or.tz under the procurement page and click the DOWNLOAD button.

6. The bidders are required to submit technical proposal (i.e. company profiles (for companies) and CVs (for individual person) describing their ability and/or capability executing the said works. All local Fundis must have a TIN number from TRA.

7. All quotations to be submitted direct through https://pass.or.tz under the procurement page and click the APPLY NOW button to upload and submit the application. As PASS Trust commitment to Inclusive Green Growth (IGG) strategy and paperless office, we will only accept electronic applications and not physical applications.

8. The deadline for submission of quotations is **17th November, 2020 at 10:00 hours.**

9. The cost of responding to this invitation to tender (IT) is to be entirely born by the bidders, whether they will be awarded or not, whether they will be invited or not to participate in further bidding procedures.

10. Late quotations portion of quotations, quotations not received, within the time specified above shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**MANAGING DIRECTOR,**
**PASS TRUST,**
**P.O BOX 9490**
**DAR ES SALAAM**

"Improving quality of life through agribusiness transformation"

# GUARDIOLA AFURAHIA KURUDI KWA JESUS



**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola alifurahishwa kuona Gabriel Jesus akifunga wakati akirudi kuichezea Manchester City ikishinda dhidi ya Olympiacos.

Jesus alitokea benchi na kufunga bao lake la kwanza tangu Septemba, akifunga kwenye ushindi wa 3-0 katika Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumanne.

Mshambuliaji huyo wa kimatafa wa Brazil amehusika kwenye mabao tisa (mabao sita na pasi za mwisho tatu) katika mechi saba zilizopita kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Guardiola, ambaye kikosi chake kitacheza na Liverpool kwenye Ligi Kuu Jumapili, alikuwa na furaha kuona nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, akifunga.

"Ilikuwa ni muhimu kwake bila shaka yoyote. Ukweli ni kwamba Gabriel amerudi na ni muhimu kwake na habari njema zaidi kwetu hasa kwa kufunga," alisema kocha huyo wa City akiwaambia waandishi wa habari.

"Kulikuwa na vitu vizuri, nilifurahishwa na muda wote wa mchezo na nina furaha kuona Gabriel amerudi."

Man City wanaongoza Kundi lao la C wakiwa na pointi tisa baada ya mechi tatu za Ligi ya Mabingwa Ulaya na wamepitwa pointi 10 na Liverpool kwenye Ligi Kuu.

# Alaba awashiwa taa ya kijani Bayern

**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich lazima ikubali kwamba, David Alaba ataondoka klabuni hapo huku Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, Hasan Salihamidzic, akiona uwezekano ni mdogo wa kufikia makubaliano.

Mkataba wa nyota huyo wa kimataifa wa Austria, unamalizika mwishoni mwa Juni na alisema Jumatatu kwamba amekatishwa tamaa na kuumizwa kwa namna klabu ilivyomchukulia.

Bayern ilibainisha kwamba imeondoa ofa iliyoiweka mezani kwa ajili ya kuongeza mkataba wa mlinzi huyo, baada ya kushindwa kufikia muafaka hadi Oktoba 31, mwaka huu.

Alaba alisisitiza kwamba hakupewa muda wa kutosha, ili kufanya maamuzi na alisikia ofa hiyo ya kuondoka kupitia vyombo vya habari.

Akizungumza baada ya ushindi wa mabao 6-2 dhidi ya Salzburg kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi, Jumanne, Salihamidzic alithibitisha kwamba Alaba ataondoka klabuni hapo hivi karibuni.

"Naweza kuwaambia nini kilichotokea. Tulikubaliana na kumpa ofa David na akakataa. Siku 10 baadaye tulikaa naye chini na kumpa ofa nyingine ikiweka muda wa mwisho," alisema Salihamidzic akiiambia Sky Sport.

"Tulimtaarifu wakala wa David kwamba tutaondoa ofa yetu muda ukifika mwisho. Na ndicho tulichokifanya.

"Nilizungumza na wakala wake tena Jumamosi na nilijaribu kuzungumza na David Jumapili kwa sababu nilitaka kujua nini kinaendelea, lakini hakuna kilichofanyika."





# *Maradona afanyiwa upasuaji*

**BUENOS AIRES,** Argentina

UPASUAJI wa ubongo aliofanyiwa Diego Maradona umefanikiwa kwa kiwango kikubwa na sasa anaendelea vizuri, kwa mujibu wa daktari wake binafsi, Leopoldo Luque.

Kocha huyo mkuu wa Gymnasia Esgrima La Plata, Maradona mwenye umri wa miaka 60, alifanyiwa upasuaji huo, Jumanne wiki hii.

Nyota huyo wa zamani wa Argentina na Napoli alikimbizwa katika hospitali ya Ipensa mjini La Plata Jumatatu, kabla ya kuhamishiwa katika Hospitali ya Olivos ya mjini Buenos Aires.

"Amefanyiwa upasuaji na sasa Diego anaendelea vizuri kabisa," alisema Luque akiwaambia waandishi wa habari. "Diego kwa sasa yupo vizuri na ataendelea kubaki hospitali kwa muda kabla ya kuruhusiwa.

"Lakini ninachoweza kuwahakikishia ni kwamba, anaendelea vizuri na kila kitu kipo sawa kwa sasa."

Maradona, ambaye ni mshindi wa Kombe la Dunia akiwa na kikosi cha Argentina mwaka 1986 pia aliisaidia Napoli kushinda mara mbili taji la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na amekuwa kocha wa Gimnasia inayoshiriki Ligi Kuu ya Argentina tangu mwaka 2019.

HABARI MICHEZO



# MESSI ASIKILIZIA OFA YA INTER

**MILAN,** Italia

LIONEL Messi hataki kuongeza mkataba wake Barcelona na sasa anafikiria ofa ya kutoka Klabu ya Inter Milan ya Italia, kwa mujibu wa OK Diario.

Messi mwenye umri wa miaka 33, amekuwa akihusishwa na kuondoka baada ya kuwasilisha maombi ya uhamisho kipindi cha majira ya joto.

Nyota huyo wa Argentina aliomba kuondoka Barcelona baada ya kuwa na msimu mbaya ambao walimaliza bila taji lolote.

Hata hivyo, mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or amekuwa akihusishwa zaidi na mpango wa kwenda kuungana na kocha wake wa zamani, Pep Guardiola kule Manchester City.

Lakini ripoti za sasa zinaeleza kwamba, Messi kwa sasa yupo tayari kusikiliza ofa kutoka Inter Milan.

Messi amebainisha wazi kabisa kwamba, hataki kuongeza mkataba pale Barcelona na ataondoka mara tu mkataba wake utakapomaliza mwishoni wa msimu huu.

Nyota huyo tangu atue pale Catalunya amekuwa na wakati mzuri akishinda mataji 10, huku manne yakiwa ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Messi pamoja na kuhuishwa na kutaka kwenda Man City, pia amekuwa akitajwa kuwaniwa na mabingwa wa Ufaransa, Paris Saint-Germain.

## Conte ajifariji kipigo cha Real Madrid

**MADRID,** Hispania

ANTONIO Conte amesema aliridhishwa na kiwango cha Inter Milan wakati wakifungwa mabao 3-2 na Real Madrid na amebaki na matumaini ya kufuzu hatua ya 16 bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Inter ililazimika kusawazisha mara mbili kwenye mchezo huo wa Jumanne uliopigwa kwenye dimba la Alfredo Di Stefano, huku Rodrygo aliyetokea benchi akifunga la ushindi kwa Madrid.

Kikosi hicho cha Conte kinashika mkia kwenye kundi lake la B kikiwa na pointi tatu na kitacheza na Madrid kwenye dimba la San Siro Novemba 25.

Licha ya Inter kushinda mechi moja kati ya saba zilizopita kwenye mashindano yote, Conte amebaki kutokuwa na wasiwasi.

"Bila shaka matokeo ya mwisho yametuacha kwenye wakati mgumu mimi na wachezaji wangu," alisema akiiambia Sport Mediaset.

"Michezo kama hii inaonyesha kwamba bado tuna nafasi ya kupambana na kurudi kwenye ubora wetu."





## Bayern yaandika historia mpya UEFA

**SALZBURG,** Ujerumani

BAYERN Munich imekuwa timu ya kwanza kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa kufunga mabao manne katika dakika 15 za mwisho, wakati wakiibuka na ushindi wa 6-2 dhidi ya Salzburg.

Bingwa huyo mtetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, mabao yake juzi, Jumanne yalifungwa na Jerome Boateng, Leroy Sane, Robert Lewandowski na Lucas Hernandez katika dakika 11 za mwisho.

Bayern ilirudi mchezoni kwa kusawazisha bao la Mergim Berisha la dakika ya nne mjini Salzburg.

Penalti ya Lewandowski ya dakika ya 21 na bao la kujifunga la Rasmus Kristensen, liliwapa vijana hao wa kocha Hansi Flick uongozi wa 2-1 katika kipindi cha kwanza.

Salzburg wakasawazisha kwa bao la Masaya Okugawa dakika ya 66 kabla ya Bayern kufunga mabao mengine manne na kupaa kileleni mwa Kundi lao la A.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RAMOS ATINGISHA KWA REKODI MABAO MADRID

Apiga la 100 na kuwa kinara kwa mabeki Ulaya, abakiza manne kumfikia Bale Madrid, huku...

**MADRID,** Hispania

NAHODHA wa Real Madrid, Sergio Ramos, ameweka rekodi ya mabao wakati Real Madrid wakiibuka na ushindi wa 3-2 dhidi ya Inter Milan kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumanne.

**Bao la kichwa alilofunga Ramos limemfanya kufikisha mabao 100 aliyofunga kwa klabu hiyo, baada ya Karim Benzema kufunga la ufunguzi.**

Lilikuwa bao lake la tisa kufunga kwa kichwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, na hivyo kumpiku John Terry na kuwa beki aliyefunga mabao mengi zaidi kwenye mashindano hayo tangu msimu wa 2003-04.

Inter ilipambana kusawazisha kwa mabao ya Lautaro Martinez na Ivan Perisic, lakini Rodrygo aliyetokea benchi alifunga la ushindi zikiwa zimesalia dakika 10 mpira kumalizika pale kwenye dimba la Alfredo Di Stefano.

Ramos alitua hapo Madrid akitokea Sevilla mwaka 2005 na amefungia mabao mengi zaidi klabu yake hiyo ya zamani.

Katika mabao yake 100 kwa Real Madrid, saba alifunga dhidi ya Sevilla, sita dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja, Atletico Madrid na matano kwenye mchezo wa Clasico dhidi ya Barcelona.

Carlos Kameni na Gorka Iraizoz ndio magolikipa aliowafunga zaidi, ambapo kila mmoja amemfunga mabao matano.

Mchezaji pekee aliyefunga mabao mengi kwa Madrid tangu alipojiunga na klabu hiyo ni Cristiano Ronaldo (450), Karim Benzema (254), Gonzalo Higuain (121) na Gareth Bale (104).

## ZISIKUPITE

### HAALAND APELEKWA LIVER

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland, mwenye umri wa miaka 20, ameungwa mkono kujiunga na Liverpool badala ya Manchester United na Mkurugenzi wa michezo wa RB Salzburg, Christoph Freund. Haaland alijiunga na Dortmund akitokea Salzburg, Januari. ***(Sky90 via Star)***

### SONG KUULA ZAIDI SPURS

MMILIKI wa Klabu ya Tottenham Hotspur, Joe Lewis, ameruhusu mshambuliaji wa Korea Kusini, Song Heung-min mwenye miaka 28, kupewa mkataba wenye thamani ya pauni 200,000 kwa wiki na marupurupu mengine. ***(Football Insider)***

### LIVERPOOL KUMKOSA SALAH

KLABU ya Liverpool inaweza kumpoteza mshambuliaji, Mohamed Salah, mwenye umri wa miaka 28, kwenye michuano tofauti msimu ujao. Kwani mchezaji huyo atakuwa na kibarua nchini Misri. ***(Ahram Online via Mirror)***

### SCHMEICHEL AISHUKIA UTD

GOLIKIPA wa zamani wa Manchester United, Peter Schmeichel, ameitaka klabu yake hiyo kuingia sokoni Januari ili kununua wachezaji wapya. ***(Bein Sports via Manchester Evening News)***

### BARCA YAMFUNGA PEDRI

BARCELONA imeweka kipengele cha uhamisho kwenye mkataba wa kiungo mshambuliaji wa Barcelona, Pedri, mwenye umri wa miaka 17 ambao ni pauni milioni 360. ***(Goal)***

### PINEDA AGOMBEWA EPL

WINGA wa Mexico na Cruz, Azul Orbelin Pineda, mwenye umri wa miaka 24, anafuatiliwa na Arsenal, Tottenham, Wolves, Everton, Southampton, Newcastle na West Ham. ***(90 min)***

### HAKUMWAZIA LAMPARD

KIUNGO wa zamani wa Chelsea na Ghana, Michael Essien, hakuwahi kuwaza mchezaji mwenzake wa zamani na kocha wa 'Blues' hao, Frank Lampard angeingia katika kazi ya ukocha. ***(Talksport)***

### CARELO KUMKUMBUKA TOSUN

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti, amemwambia mshambuliaji wa Uturuki, Cenk Tosun mwenye umri wa miaka 29, kuwa atatumika katika "michezo kadhaa" msimu huu, baada ya kuonekana mara ya kwanza dhidi ya Newcastle mwishoni mwa juma lililopita katika kipindi cha miezi 11. ***(Liverpool Echo)***

### MILAN BADO KWA EMERSON

AC Milan imemfanya mlinzi wa Barcelona, Emerson mwenye umri wa miaka 21, ambaye anacheza kwa mkopo katika klabu ya Real Betis, kuwa mchezaji wanayemhitaji zaidi msimu ujao. ***(Todofichajes)***

### SARRI ANUKIA FIORENTINA

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Maurizio Sarri, anaongoza katika orodha ya watakaochukuwa nafasi ya Bappe Lachini kama atafukuzwa kule Fiorentina. ***(Calciomercato)***

HABARI MICHEZO

## Tigo kuuza tiketi za ligi kidigitali

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Kimtandao (NIDC), zimeungana kwa ajili ya kuwarahisishia mashabiki wa soka kununua tiketi kwa njia ya Tigo Pesa katika michezo mbalimbali itakayochezwa Uwanja wa Uhuru na Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Kaimu Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Peter, alisema wameungana na NIDC kwa ajili ya kuwasaidia mashabiki wa soka kuondokana na msongamano wakati wa kukata tiketi kwa kutumia njia ya mtandao.

Alisema mashabiki wa soka kwa sasa watakuwa wamepunguza suala la kutembea na fedha taslimu na badala yake wataanza kutumia huduma ya kukata tiketi kwa njia ya Tigo Pesa.

"Tanzania ni moja ya nchi za kuigwa katika kufanya malipo kielektroniki. Kupitia malipo haya ya N-Card tumeendelea kupeperusha bendera katika nyanja ya malipo ya kidigitali," alisema Angelica.

Ofisa Uhusiano wa Kituo cha NIDC, Geophrey Mlelwa, alisema wamefurahia kuungana na Tigo kwa ajili ya kuleta mapinduzi kwenye michezo.

## Zanzibar yataja kikosi cha U-20

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limetangaza kikosi cha wachezaji 25 watakaounda timu ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (U-20), ambacho kinajiandaa na mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika baadaye mwezi huu jijini Arusha.

Kaimu Katibu wa Kamati ya Soka la Vijana ya ZFF, Mohamed Seif 'King', alisema katika kujiandaa na mashindano hayo, timu hiyo itacheza mechi mbili za kirafiki ikiwa visiwani Zanzibar kwa lengo la kuwaweka tayari na michuano hiyo.

King alisema mechi ya kwanza itachezwa Novemba 15, mwaka huu na marudiano yatafanyika Novemba 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa Amaan na wageni wao yosso kutoka Sudan watawasili nchini Novemba 12, mwaka huu.

Aliwataja wachezaji walioitwa kwenye timu hiyo ni pamoja na magolikipa, Arjif Omar kutoka Hard Rock, Hamadi Ubwa (Mlandege) na Abdulratif Masoud wa Jamhuri huku walinzi wakiwa ni Abdallah Lasso (Mlandege), Abdulhamid Ali (JKU Academy), Kassim Hassan (Mafunzo), Nassor Azan (Malindi), Mohamed Shaa (Jang'ombe Boys), Mudathir Ali (Zimamoto) na Ibrahim Juma wa Mwembe Makumbi Academy.

Viungo ni Jamel Jaku (Azam U-20), Paschal Daudi (ZFDC), Habil Massoud (Huru), Kassim Suleiman Mchobwa (Zimamoto U-20), Khalid Shaban (KMKM), Ali Ali (Mlandege U-20), Aboubakar Bakari (Coast City) na Ibrahim Mnyaa wa New Africa.

Mastraika ni Abas Rajab (Raskazone), Mohmed Maulid (Mapembeani), Mudrick Sheshe (JKU), Suleiman Ali (Hard Rock ), Fahad Mussa (Mlandege), Yusuf Bwanga (ZFDC) na Ali Salum Ali kutoka Kilimani City.

# KATWILA ATAKA REKODI YA MTIBWA IHEFU FC

**Na Saada Akida**

WAKATI timu yake ikiburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila, amesema atapambana kuhakikisha analinda rekodi yake kabla mzunguko wa kwanza haujamalizika.

**Akizungumza na gazeti hili akiwa njiani kuelekea Sumbawanga, Katwila alisema ana imani na wachezaji wake wataongeza bidii ili timu yao ipate pointi na kujiweka kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi hiyo.**

Katwila alisema mipango yake ni kuona anaendeleza rekodi yake ya kufanya vema kwenye ligi kama alivyokuwa akiaminiwa na klabu yake ya zamani, Mtibwa Sugar.

"Msimu uliopita nilipokuwa Mtibwa, walisema tunashuka, kama wanavyosema sasa ila ninachokiamini ni kwamba tuna uwezo wa kufanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yetu na kutoka hapa tulipo sasa," alisema Katwila.

Aliongeza ameikuta Ihefu ikiwa katika nafasi ya chini, lakini anaamini wachezaji walioko wana nafasi ya kupambana na hatimaye kupata matokeo mazuri kwa kuanza na Tanzania Prisons.

"Tunaenda kucheza ugenini, tunawaheshimu wapinzani wetu na tutaingia uwanjani kwa tahadhari kubwa kwa sababu upande wetu tunahitaji kupata pointi muhimu zaidi na wao wakitafuta heshima uwanja wa nyumbani," alisema Katwila.

Aliongeza kuwa, kwa sasa analazimika kuwajenga wachezaji waliopo ili kusaka ushindi, lakini dirisha dogo litakapofunguliwa, atasajili nyota wapya kulingana na mahitaji.

"Kwa sasa nawajibika kutumia 'askari' nilionao, si wabaya, ila kuna wakati mpira una matokeo yasiyotarajiwa, unacheza sana na unapoteza mchezo, unapambana kiasi unavuta pointi tatu au mnagawana pointi, ila hatutakata tamaa, tutapambana kwa ajili ya kuibakisha timu," Katwila alisema.

Tanzania Prisons itaikaribisha Ihefu katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga.

USHINDI...



Wachezaji wa timu ya Mbeya Kwanza, wakishangilia baada ya kupata bao la kuongoza wakati wakishinda 2-0 dhidi ya Gipco FC kwenye mechi ya Ligi Daraja la Kwanza Kundi A iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam Jumatatu wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mwakinyo aongeza 'dozi' ya mazoezi*

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha anaimarika zaidi na kumpiga mpinzani wake, Jose Carlos Paz kutoka Argentina, bondia maarufu nchini, Hassan Mwakinyo, amebadili ratiba ya mazoezi na sasa anajifua kwa saa nne kwa siku.

Mwakinyo ambaye ameweka kambi katika eneo la Magoroto, Muheza jijini Tanga, anajiandaa kuwania ubingwa wa mabara wa WBF na kuwania ubingwa mpya wa mabara wa IBA wa uzito wa Super-welter.

Bondia huyo anajifua chini ya Kocha, Hamis Mwakinyo, pamoja na wasaidizi mbalimbali huku wakitumia video mbalimbali kumsoma Paz ambaye ana rekodi nzuri.

"Nimehama nyumbani na kujichimbia huku Magoroto kwa lengo la kufanya vema katika pambano hilo, kujifua zaidi ya raundi 12 ili kupata stamina ya kwenda sambamba na mpinzani wangu," alisema Mwakinyo.

Katika hatua nyingine, waandaaji wa pambano hilo wamesema kuwa bondia Paz anatarajiwa kuwasili nchini leo huku tiketi kwa ajili ya pambano hilo zikiuzwa mtandaoni kupitia Kampuni za Nilipe na Selcom.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Jackson Group Sports, Kelvin Twissa, alisema mbali ya Mwakinyo na Paz, pia siku hiyo kutakuwa na mapambano mengine ambapo bondia nyota wa kike, Zulfa Macho atazipiga na Alice Mbewe kutoka Zambia wakati Hussein Itaba atazichapa na Alex Kabangu katika uzito wa Super-Middle.

Twisa alisema pia Mkenya, Fatuma Zarika atazichapa na Patience Mastara wa Zimbawe katika uzito wa Super Bantam.

"Paz ameamua kuwasili mapema Tanzania ili kuzoea hali ya hewa, katika msafara wake yupo kocha wake, Oscar Alberto Ramon," Twisa aliongeza.

# Michezo

Alhamisi Novemba 5, 2020

Nipashe




Ramos atingisha rekodi mabao Madrid

UKURASA 22

WAMEKUBALI...



Wachezaji wa Simba, wakishangilia baada ya kupata bao la pili dhidi ya Kagera Sugar, lililozamishwa kimyani kwa shuti kali na Hamis Ndemla (aliyembeba Hassan Dilunga) wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA SC NA MOTO MKALI KWA YANGA

●●● Kagera Sugar yageuzwa 'Kijumbe' Uhuru, yawaita mashabiki kwa Mkapa Jumamosi huku...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU ikikosa mabao mengi kipindi cha kwanza, timu ya Simba jana 'iliigeuza' Kagera Sugar 'Kijumbe' wa kufikisha salamu zao kwa watani zao, Yanga kuelekea mechi ya 'Dabi ya Dar es Salaam' Jumamosi, baada ya kuwachapa 'Walima Miwa' hao wa Kagera kwa mabao 2-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Uhuru.

**Yanga ambayo ililazimishwa sare tasa juzi na Gwambina FC ikiwa Misungwi, Mwanza, hivyo kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 23, Jumamosi itaikaribisha Simba katika Uwanja wa Mkapa.**

Kwa matokeo hayo ya Simba, sasa inafikisha pointi 19 katika nafasi ya tatu ikizidiwa pointi tatu na Azam FC iliyopo nafasi ya pili.

Mabao ya John Bocco kwa mkwaju wa penalti dakika ya 42, huku dakika za majeruhi kipindi cha kwanza Said Ndemla akifunga la pili kwa timu yake, hilo likiwa pia ni bao lake la pili msimu huu akifunga mfululizo, baada ya mechi iliyopita dhidi ya Mwadui FC kuziona nyavu wakati wakishinda 5-0 katika uwanja huo.

Simba ilianza mechi kwa nguvu, lakini ikikosa mabao mfululizo na kusababisha mashabiki wake kuingiwa na hofu ya kufanya vema kwenye mechi hiyo.

Dakika ya nane tu, nahodha Bocco alikosa bao alipopiga kichwa mpira wa faulo iliyopigwa na Mohamed Hussein 'Tshabalala' na kutoka nje. Ibhahim Ajibu naye dakika ya 17 akiwa yeye na kipa Benedict Tinoko, alipiga shuti hafifu na kupanguliwa na mlinda mlango huyo, baada ya pasi ya kichwa kutoka kwa Bocco.

Hassan Dilunga alikuwa miongoni mwa wachezaji waliokosa mabao ya wazi, baada ya kukokota mpira kwa umbali mrefu dakika ya 25, lakini shuti lake liliwekewa mguu na beki David Luhende na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Bocco tena akiwa yeye na kipa, alipiga shuti dhaifu la mguu wa kushoto, mpira ukaokolewa na kipa Tinoko ambaye alifanya kazi kubwa kwenye mechi hiyo kuzuia mashambulizi mengi ya Simba.

Dakika ya 35, Dilunga tena alipiga shuti lililookolewa kwa mguu na kipa huyo. Hatimaye Kagera Sugar ilifanya shambulizi kubwa dakika ya 35 baada ya mfungaji wao tegemeo Yusuph Mhilu kumuacha Shomari Kapombe na kuachia shuti kali lililombabatiza beki wa Simba Ibrahim Ame na kuwa kona.

Dilunga aliangushwa ndani ya eneo la hatari na David Luhende wakati akiambaa kumuona Tinoko na kusababisha penalti dakika ya 42, iliyowekwa wavuni kwa ustadi na Bocco.

Wakati kila mmoja akidhani mechi hiyo ingekwenda mapumziko Simba ikiongoza kwa bao moja pekee, Ndemla alimegewa pande safi na 'Master pasi', Clatous Chama, akaachia kombora kali la karibu na mpira kujaa wavuni.

Kipindi cha pili Kagera Sugar walicharuka kutaka kurudisha mabao hayo, huku Simba ikionekana kucheza kwa tahadhari kwa ajili ya mechi ya Jumamosi dhidi ya Yanga, lakini washambuliaji wa timu hiyo, Mhilu, Vitalis Mayanga na Nassor Kapama, harakati zao ziliishia kwa mabeki wa kati Ame na Joash Onyango ambao walikuwa hawataki masihara langoni mwao.

Nadhodha aliyebaki na kitambaa hadi mechi inamalizika, Shomari Kapombe, baada ya mechi alieleza kufurahishwa na ushindi huo, lakini akisema akili zao zote zinaelekezwa Jumammosi kwenye mechi ya dhidi ya watani zao.

"Hakuna mchezaji ambaye hapendi kucheza mechi kubwa, tumejiandaa na mechi hiyo na tunawaomba mashabiki wetu waje kwa wingi kutupa sapoti kwenye mechi hiyo kwa sababu sisi tunawategemea nao wanatutegemea," alisema Kapombe aliyechiwa kitambaa cha unahodha na Chama kabla ya kutoka, ambaye naye aliachiwa na Bocco alipokuwa akitoka.

## Wachezaji wanaitaka dabi-Kaze

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema wachezaji wake wanahamu sana ya kucheza mechi ya watani wa jadi, Simba itakayopigwa keshokutwa, Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kulazimishwa sare tasa dhidi ya Gwambina FC katika mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Gwambina, Misungwi nje kidogo ya Jiji la Mwanza, Kaze alisema siku zilizobaki kabla ya mechi hiyo zinawatosha kujiandaa vizuri kukabiliana na watani zao.

"Tumetoka kwenye mechi ngumu tunakwenda kujiandaa na mechi ngumu, tuna siku nne (kuanzia juzi) za kujiandaa, kila mchezaji ana hamu ya kucheza mechi hiyo ambayo itatazamwa na Watanzania wengi ndani na nje ya nchi," alisema kocha huyo raia wa Burundi.

Kuhusu mabadiliko ya wachezaji tisa aliyoyafanya katika kikosi kilichocheza dhidi ya Gwambina kutoka walioanza mechi dhidi ya Biashara United kuwa ni mbinu ya kuwapumzisha nyota wake kwa ajili ya kusubiri 'dabi' hiyo ya Dar es Salaam dhidi ya Simba, Kaze alipinga huku akieleza ni kutokana na ugumu wa ratiba.

"Mechi ijayo itakuwa ni ngumu, hasa ukizingatia timu imetoka kucheza mechi ngumu, hatukuweza kuchezesha wachezaji mechi zote nne ndani ya siku 12," alisema.

Kuhusu sare ya juzi, alisema wapinzani wao 'walipaki basi' kitu ambacho kiliwapa ugumu kufungua njia za kwenda kupata mabao, huku pia akilia na uwanja ambao haukuwa rafiki kwao kutengeneza nafasi za mabao.

"Walikaa nyuma muda mrefu, halafu wakawa wanajiangusha na kuumia mara kwa mara kwa lengo la kupoteza muda, hali ya uwanja haikuwa nzuri pia, lakini pamoja na yote hayo si sababu ya asilimia zote za sisi kutokupata ushindi, ingawa hii nayo imechangia, " alisema.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >